# IDARA YA ELIMU JIMBO LA KANSAS
# HAKI ZA WAZAZI KATIKA ELIMU MAALUM
# (Taratibu za Ulinzi)

Wewe pamoja na shule mna jukumu la kutekeleza katika elimu ya mtoto wako. Ikiwa wewe au shule mna suala au dukuduku kuhusu elimu ya mtoto wako, mwalimu wa mtoto wako pamoja nawe lazima mjadili masuala hayo kwa uwazi. Ikiwa hujaridhika na mazungumzo hayo, unapaswa kuwasiliana na mkurugenzi wa elimu maalum katika wilaya yako ya shule. Tunakuhimiza ushiriki kikamilifu katika elimu ya mtoto wako.

Kama wazazi wa watoto ambao, au huenda, ni wa kipekee, mna haki fulani au taratibu za ulinzi chini ya sheria za serikali ya taifa. Haki hizi zimeorodheshwa katika Ilani hii ya *Taratibu za Ulinzi.* Ni sharti upewe orodha hii ya haki zako kwa lugha yako asili au kwa njia ya mawasiliano unayoweza kuelewa. Ikiwa ungependa maelezo zaidi ya haki hizi, tafadhali wasiliana na mkuu washule ya mtoto wako, msimamizi wa shule, mkurugenzi wa elimu maalum, au Idara ya Elimu Jimbo la Kansas (KSDE), 900 SW Jackson St. Suite 620 , Topeka , KS 66612; simu (800) 203-9462. Nakala za haki hizi katika maandishi ya Nukta Nundu, kanda za sauti na lugha nyingine zinapatikana kutoka shule yako ukiomba upewe. Kwa maelezo zaidi kuhusu haki zako, unaweza kuomba nakala ya Mwongozo wa Elimu Maalum kutoka *Families United, Inc* .: Wichita 1-888-815-6364 au (316) 945-7747 Sauti/ TTY; Garden City 1-888-820-6364 au (620) 276-6364 Sauti/TTY; Topeka 1-800-264-6343 au (785) 233-4777; Kansas City 1-877-499-5369 au (913) 287-1970 au Idara ya Elimu Jimbo la Kansas (800) 203-9462. Aidha, Kitabu cha Mafunzo ya Mchakato wa Elimu Maalum Kansas kinapatikana kwenye tovuti ya Idara ya Elimu Jimbo la Kansas kwenye www.ksde.org.

## Ilani ya Taratibu za Ulinzi

Ilirekebishwa Agosti 2010

Sheria ya Uboreshaji wa Elimu ya Watu wenye Ulemavu (IDEIA), ambayo ni sheria ya Taifa kuhusu elimu ya wanafunzi wenye ulemavu, inazitaka shule zikupe wewe, mzazi wa mtoto mwenye ulemavu, taarifa iliyo na maelezo kamili kuhusu taratibu za ulinzi unaopatikana chini ya IDEA na kanuni za Wizara ya Elimu ya Marekani. Lazima upewe nakala ya ilani hii mara moja tu katika mwaka wa shule, ingawa pia lazima upewe nakala: (1) mara ya kwanza unapoelekezwa shuleni au unapooomba tathmini; (2) baada ya kupokea malalamiko ya kwanza ya Serikali chini ya 34 CFR §§300.151 kupitia 300.153 na baada ya kupokea malalamiko ya mchakato wako wa kwanza chini ya §300.507 katika mwaka wa shule; (3) wakati uamuzi unafanywa kumchukulia mtoto wako hatua za nidhamu inayohusu mabadiliko ya kuwekwa chini ya §300.536; na (4) baada ya ombi lako. [34 CFR §300.504(a)]

Ilani hii ya utaratibu wa ulinzi lazima ijumuishe ufafanuzi kamili wa utaratibu wa ulinzi unaopatikana chini ya §300.148 (uamuzi wa moja kwa moja kumweka mtoto katika shule binafsi kwa gharama za umma), §§300.151 kupitia 300.153 (taratibu za Serikali za malalamiko), §300.300 (kibali cha wazazi ) § §300.502 na 300.503 (Tathmini Huru ya Mahitaji ya Kielimu na taarifa ya awali kwa maandishi), §§300.505 hadi 300.518 (taratibu nyingine za ulinzi, kwa mfano, usuluhishi, mchakato rasmi wa malalamiko, mchakato wa utatuzi na utaratibu usioegemea upande wowote wa kusikiliza), §§300.530 hadi 300.536 (taratibu za ulinzi katika sehemu ya chini ya E ya Kanuni ya B juu ya vitendo vya kisheria) na §§300.610 kupitia 300.625 (usiri wa masharti ya taarifa katika sehemu ya F).

## Taarifa Kuhusu Masharti Yaliyowekwa na Serikali Haihitajika kwa Sehemu ya B ya sheria ya IDEA au Kanuni zake za Utekelezaji

Kwa mujibu wa sheria za taifa, katika kipengele cha 34 CFR 300.199 (a) (2), hii taarifa iliyoandikwa ya matakwa ya ziada yaliyowekwa na serikali, ambayo hayahitajika kwa Sehemu ya B ya IDEA au kanuni zake za utekelezaji. Matakwa ya Serikali yanatambuliwa kwa alama ya nyota (*) na itakuwa na itarejelea sheria na kanuni za Kansas, zinazoonyeshwa kwa maandishi K.S.A au K.A.R.

# Yaliyomo

**Maelezo ya Jumla**

- *Nyenzo Zinazoweza Kulinganishwa na Zinazofaa Umri
- *Taratibu za Kutathmini
- *Ripoti ya Tathmini
- Taarifa ya Awali kwa Maandishi
- Lugha Asili
- Barua Pepe
- *Aina za Upekee
- *Malengo ya Baada ya Elimu ya Sekondari na Huduma za Mpito
- Kibali cha Mzazi - Ufafanuzi
- Kibali cha Mzazi
- *Kibali cha Mzazi kwa Mabadiliko ya Muhimu katika Huduma au Mabadiliko Makubwa yanayohusu Mahali Mtoto Anaposoma
- *Kubatilisha Kibali kwa Huduma Mahususi
- Tathmini Huru ya Mahitaji ya Kielimu

**Usiri wa Taarifa**

- Fasili
- Sifa Tambulishi
- Taarifa kwa Wazazi
- Haki za Kupata
- Kufikia Rekodi
- Rekodi za Zaidi ya Mtoto Mmoja
- Orodha ya Aina na Sehemu Taarifa Zilipo
- Ada
- Marekebisho ya Kumbukumbu kwa Ombi la Mzazi
- Fursa ya Kusikilizwa
- Utaratibu wa Kusikilizwa
- Matokeo ya Kusikilizwa
- Ruhusa ya Kufichua Taarifa za Sifa Tambulishi
- Ulinzi
- Kuharibu Taarifa

**Utaratibu wa Malalamiko ya Serikali**

- Tofauti kati ya Utaratibu wa Malalamiko na Kusikilizwa kwa Kufuata Mchakato na Malalamiko ya Serikali
- Taratibu za Kupokea Malalamiko ya Kiserikali
- Kima cha Chini kwa Utaratibu wa Malalamiko ya Kiserikali
- Kuwasilisha Malalamiko ya Serikali

**Utaratibu wa Malalamiko Yanayofuata Mchakato**
- Kuwasilisha Malalamiko Yanayofuata Mchakato
- Malalamiko Yanayofuata Mchakato
- Fomu za Mifano
- Usuluhishi
- Mchakato wa Utatuzi

**Kusikiliza Malalamiko Yanayofuata Mchakato**
- Utaratibu Huru wa Kusikiliza Malalamiko Yanayofuata Mchakato
- Haki za Kusikilizwa
- Maamuzi ya Kusikilizwa

**Rufaa**
- Ukamilifu wa Uamuzi; Rufaa; Ukaguzi Huria
- Muda na Urahisi wa Kusikilizwa na Ukaguzi
- Mashtaka ya Kiraia, Ikiwemo Kipindi cha Muda wa Kuanzisha Mashtaka Hayo
- Kituo cha Mtoto Wakati wa Kusubri Utaratibu wa Malalamiko na Kusikilizwa kwa Kufuata Mchakato
- Ada za Wakili

**Utaratibu wa Kuwaadhibu Watoto wenye Ulemavu**
- Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule
- Mabadiliko ya Mahali pa Kusoma kwa Sababu za Nidhamu
- Uamuzi wa Mazingira
- Rufaa
- Mahali pa Kusomea Wakati wa Rufaa
- Ulinzi kwa Watoto Wasiostahiki Elimu Maalum na Huduma Zinazohusiana
- Kuelekezwa pamoja na Hatua Zinazochukuliwa na Maofisa wa Utekelezaji wa Sheria na Mahakama

**Masharti ya Kuchukua Uamuzi wa Moja kwa Moja Unaochukuliwa na Wazazi wa Watoto walio katika Shule za Binafsi kwa Gharama za Umma**
- Masharti ya Serikali ya Taifa kwa Watoto Waliosajiliwa katika Shule za Binafsi kwa Hiari
- *Masharti ya Jimbo kwa Watoto Waliosajiliwa katika Shule za Binafsi kwa Hiari
- Tatizo Linapohusu Elimu Inayofaa ya Umma Bila Malipo

# MAELEZO YA JUMLA

## *NYENZO ZINAZOWEZA KULINGANISHWA NA ZINAZOFAA UMRI

**K.A.R. 91-40-52(d)**

Vifaa vyote kwa ajili ya watoto wa wenye mahitaji ya kipekee vinapaswa kuwa sawa na vya watoto wasio na mahitaji ya kipekee. Aidha, vituo vyote vya watoto walio na mahitaji ya kipekee vinapaswa kuwa na mazingira yanayofaa. Kila mazingira lazima yawe sahihi kwa mpango wa mafunzo yanayotolewa.

## *TARATIBU ZA KUTATHMINI

**K.A.R. 91-40-7(c)**

Bodi inaweza kumwelekeza mtoto ambaye amesajiliwa katika shule ya umma kwa tathmini ikiwa moja ya masharti yafuatayo yametimizwa:

1. Wafanyakazi wa shule wana nyaraka zinazotokana na data ambazo zinaonyesha kwamba mipango na mikakati ya kawaida ya elimu haitahudumia mahitaji maalum ya mtoto;

2. Wafanyakazi wa shule wana nyaraka zinazotokana na data zinaonyesha kuwa kabla ya kumwelekeza mtoto au kama sehemu ya uelekezaji, hali zote zifuatazo zimetimizwa: (a) mtoto alipewa mafunzo sahihi katika mazingira ya kawaida ya elimu iliyotolewa na wafanyakazi wenye weledi; (b) mafanikio ya kielimu ya mtoto yalipimwa mara kwa mara kwa muda unaofaa uliolingana na tathmini rasmi ya maendeleo ya mwanafunzi wakati wa mafunzo; (c) matokeo ya tathmini yalitolewa kwa mzazi au wazazi wa mtoto; (d) matokeo ya tathmini yanaonyesha kwamba tathmini ni sahihi au

3. Mzazi wa mtoto ameomba na akatoa idhini kwa maandishi kuruhusu mtoto afanyiwe tathmini na bodi imekubaliana kwamba mtoto anafaa kufanyiwa tathmini.:

## *RIPOTI YA TATHMINI

**K.A.R. 91-40-10(a)**

Ripoti ya tathmini iliyoandikwa inahitajika baada ya kukamilika kwa tathmini yoyote au tathmini mpya, bila kujali aina ya mahitaji maalum yanayoshukiwa

## TAARIFA YA AWALI KWA MAANDISHI

**34 CFR §300.503**

**Taarifa**

Wilaya husika ya shule inapaswa kukupa taarifa iliyoandikwa (ikupe maelezo fulani kwa maandishi), ndani ya muda wa kutosha kabla:

1. Ipendekeze kuanzisha au kubadili utambulisho, tathmini, au mahali pa mtoto wako kusoma, au utoaji wa elimu inayofaa ya umma bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako; **au**

2. Ikate kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini, au mahali pa mtoto wako kusoma au utoaji wa FAPE kwa mtoto wako.

**Maudhui ya taarifa**

Taarifa iliyoandikwa lazima:

1. Ieleze hatua ambayo wilaya yako ya shule inapendekeza au inakataa kuchukua;

2. Ieleze kwa nini wilaya yako ya shule inapendekeza au kukataa kuchukua hatua;

3. Ieleze utaratibu wa kila tathmini, mtahani, rekodi, au ripoti iliyotumiwa na wilaya yako ya shule kuamua au kukataa hatua;

4. Ijumuishe taarifa kwamba unalindwa chini na vipengele vya taratibu za ulinzi katika Sehemu B ya IDEA;

5. Ikuambie jinsi unavyoweza kupata maelezo ya utaratibu wa ulinzi ikiwa hatua ambayo wilaya yako ya shule inapendekeza au kukataa si tathmini ya mwanzo wa mtoto kuelekezwa kwingine;

6. Ijumuishe watu unaoweza kuwasiliana nao ili wakusaidie kuelewa Sehemu ya B ya IDEA;

7. Ieleze chaguo nyinginezo ambazo Timu ya Mpango Mahususi kwa Elimu ya Mtoto (IEP) ilizingatia na sababu za kukataliwa kwa chaguo hizo; **na**

8. Itoe maelezo ya sababu nyingine zilizofanya wilaya yako ya shule ipendekeze au ikataehatua.

**Taarifa iwe katika lugha inayoeleweka**

Taarifa lazima iwe:

1. Imeandikwa kwa lugha inayoeleweka kwa umma kwa ujumla; **na**

2. Inapatikana katika lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano unayotumia, isipokuwa kama ni wazi kuwa haiwezekani kufanya hivyo.

Ikiwa lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano si lugha inayoandikwa, wilaya yako ya shule lazima ihakikishe kuwa:

1. Taarifa inatafsiriwa kwako kwa matamshi au kwa njia nyingine katika lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano;

2. Unaelewa yaliyo kwenye taarifa; **na**

3. Kuwe na ushahidi ulioandikwa kwamba masharti ya aya ya 1 na 2 yametimizwa.

## LUGHA ASILI

**34 CFR §300.29**

*Lugha asili,* inapotumiwa kumrejelea mtu asiyefahamu Kiingereza sana, ina maana ifuatayo:

1. Lugha ambayo mtu huyo hutumia kwa kawaida, au, kama ni mtoto, lugha ambayo kwa kawaida hutumiwa na wazazi wa mtoto;

2. Katika mawasiliano yote ya moja kwa moja na mtoto (ikiwa ni pamoja na wakati wa tathmini ya mtoto), lugha ambayo kawaida hutumiwa na mtoto katika mazingira ya nyumbani au kujifunza.

Kwa mtu aliye na uziwi au upofu, au kwa mtu asiye na lugha iliyoandikwa, njia ya mawasiliano ni ile ambayo mtu huyo hutumia kwa kawaida (kama lugha ya ishara, nukta nundu, au mawasiliano kwa mazungumzo).

## BARUA PEPE

**34 CFR §300.505**

Ikiwa wilaya yako ya shule inawapatia wazazi chaguo la kupokea nyaraka kwa barua pepe, unaweza kuchagua kupokea yafuatayo kwa barua pepe:

1. Taarifa ya awali kwa maandishi;

2. Taarifa ya taratibu za ulinzi; **na**

3. Arifa zinazohusiana na malalamiko yanayofuata mchakato

## *AINA ZA UPEKEE

**K.S.A. 72-962(g)**

Makundi ya upekee uliojumuishwa katika sheria na kanuni za elimu maalum Kansas ni pamoja na jamii ya watoto wenye "vipawa" ambao ni umri wa kwenda shule. .

## *MALENGO YA BAADA YA ELIMU YA SEKONDARI NA HUDUMA ZA MPITO

**K.S.A. 72-987(c)(8) and K.A.R. 91-40-1(uuu)**

Kuanzia umri wa miaka 14 na kurekebishwa kila mwaka baada ya hapo, Mpango Mahususi wa Elimu (IEP) ya mtoto mwenye ulemavu lazima ijumuishe: (a) malengo ya yanayopimika ya baada ya elimu ya sekondari yanayolingana na tathmini ya mabadiliko ya umri, mafunzo, elimu, kazi na ikiwa inafaa, ujuzi wa kuweza kujitegemea; na (b) huduma za mpito, ikiwa ni pamoja na kozi zinazofaa, zinahitajika kumsaidia mtoto afikie malengo ya baada ya masomo ya sekondari.

## KIBALI CHA MZAZI - UFAFANUZI

**34 CFR §300.9**

**Kibali**

Kibali ina maana kwamba:

1. Umejulishwa kikamilifu katika lugha yako asili au njia nyingine ya mawasiliano (kama vile lugha ya ishara, nukta nundu, au mawasiliano ya mdomo) kuhusu taarifa zote za hatua unayotolea kibali.
2. Unaelewa na unakubali kwa maandishi hatua hiyo na kwamba kibali chako kinaelezea hatua hiyo na kuorodhesha rekodi (ikiwa zipo) ambazo zitatolewa na kwa nani; **na**
3. Unaelewa kwamba kibali chako ni kwa hiari na kwamba unaweza kughairi kibali chako wakati wowote.

Ikiwa unataka kubatilisha (kughairi) kibali baada ya mtoto wako kuanza kupata elimu maalum na huduma zinazohusiana, lazima ufanye hivyo kwa kuandika. Kubatilisha kibali chako hakubadili (kufuta) hatua iliyofanyika baada ya kutoa idhini yako lakini ikaighairi baadaye. Aidha, wilaya ya shule haitakiwi kurekebisha (kubadilisha) rekodi za elimu ya mtoto wako ili kuondoa kumbukumbu yoyote kwamba mtoto wako alipokea elimu maalum na huduma zinazohusiana baada ya kubatilisha kibali chako.

## KIBALI CHA MZAZI

**34 CFR §300.300**

**Kibali cha tathmini ya awali**

Wilaya husika ya shule haiwezi kufanya tathmini ya awali ya mtoto wako ili kujua kama mtoto wako ana haki chini ya Sehemu B ya Sheria ya Uboreshaji wa Elimu ya Watu wenye Ulemavu (IDEIA), kupata elimu maalum na huduma zinazohusiana bila ya kwanza kukupa taarifa ya awali kwa maandishi kuhusu hatua inayopendekezwa na kupata kibali chako kama inavyoelezwa katika mada yenye kichwa ***Taarifa ya Awali kwa Maandishi*** na ***Kibali cha Mzazi.***

Wilaya yako ya shule lazima ifanye jitihada za kutosha kupata kibali chako kinachotokana na ufahamu kwa ajili ya tathmini ya awali ili kuamua ikiwa mtoto wako ni mtoto mwenye ulemavu.

Kibali chako cha tathmini ya awali haimaanishi kwamba umetoa idhini kwa wilaya ya shule ianze kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mtoto wako.

Wilaya ya shule haitatumia kukataa kwako kukubali huduma moja au shughuli zinazohusiana na tathmini ya kwanza kama msingi wa kukataa wewe au mtoto wako kupokea huduma yoyote, manufaa au shughuli, isipokuwa Sehemu nyingine ya B inaitaka wilaya ya shule ifanye hivyo .

Ikiwa mtoto wako amejiunga na shule ya umma au unataka mtoto wako ajiunge na shule ya umma na umekataa kutoa kibali au hukujibu ombi la kutoa kibali cha tathmini ya awali, wilaya yako ya shule inaweza, ingawa si lazima, kumfanyia mtoto wako tathmini ya awali kwa kuzingatia usuluhishi wa sheria ya IDEA au malalamiko yanayofuata mchakato, mkutano wa kuelewana, na utaratibu wa kusikilizwa katika mchakato huria. Wilaya yako ya shule itakuwa haitakiuka majukumu yake ya kutafuta, kutambua na kumtathmini mtoto wako ikiwa haifanya tathmini ya mtoto wako katika hali hii.

**Kanuni maalum kwa ajili ya tathmini ya awali ya watoto wa Serikali**

*Watoto wa Serikali* , kama inavyotumika katika sheria ya IDEA, ina maanisha ya mtoto ambaye, kama inavyoelezwa na Jimbo ambapo mtoto anaishi, ni: 1. Mtoto anayelelewa wasio wazazi wake; 2. Anachukuliwa kuwa mtoto wa Serikali chini ya sheria za Jimbo; **au** 3. Inakaa katika makao ya shirika la umma la ustawi wa watoto. (*Watoto wa Serikali* hawajumuishi mtoto aliye na mzazi mlezi ambaye kwa mujibu wa ufafanuzi unaotumiwa na sheria ya IDEA ni *mzazi*.)

Ikiwa mtoto anachukuliwa kuwa mtoto wa Serikali na haishi na mzazi wake — Wilaya ya shule haina haja ya kupata kibali kutoka kwa mzazi ili kufanya tathmini ya awali ya kubaini kama mtoto ni mtoto mwenye ulemavu ikiwa:

1. Licha ya jitihada za kutosha, wilaya ya shule haiwezi kupata mzazi wa mtoto;
2. Haki za wazazi zimekatizwa kwa mujibu wa sheria ya Jimbo; **au**
3. Jaji amempa haki ya kufanya maamuzi ya elimu mtu mwingine ambaye si mzazi na kwamba mtu huyo ametoa kibali kwa ajili ya tathmini ya awali.

**Kibali cha mzazi kuhusu huduma**

Wilaya yako ya shule lazima ipate kibali chako kabla ya kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza.

Wilaya ya shule lazima ifanye jitihada za kutosha kupata kibali chako kabla ya kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza.

Ikiwa hutajibu ombi la kutoa kibali ili mtoto wako apate elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, au ukikataa kutoa kibali hicho au ubatilishe (kughairi) kibali chako kwa maandishi, wilaya yako ya shule haiwezi kutumia taratibu za ulinzi (yana ni, usuluhishi, malalamiko yanayofuata mchakato, mkutano wa utatuzi, au kusikilizwa katika mchako huria) ili kupata kibali au maamuzi kuwa mtoto wako anaweza kupewa elimu maalum na huduma zinazohusiana (inayopendekezwa na Timu ya IEP ya mtoto wako) bila idhini yako.

Ukikataa kutoa kibali ili mtoto wako apate elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, au ikiwa hutajibu ombi la kutoa idhini hiyo au baadaye ubatilishe (kughairi) idhini yako kwa kuandika halafu wilaya ya shule isimpe mtoto wako elimu maalum na huduma zinazohusiana ambayo iliyotaka idhini yako kuihusu, basi wilaya yako ya shule:

1. Itakuwa haijakiuka matakwa ya kufanya elimu inayofaa ya umma bila malipo (FAPE) ipatikane kwa mtoto wako kwa kushindwa kutoa huduma hizo kwa mtoto wako; na

2. Haitakiwi kuwa na mkutano wa mpango mahususi wa elimu ya mtoto (IEP) au kuandaa IEP ya mtoto wako kwa ajili ya elimu maalum na huduma zinazohusiana ambayo ulikuwa umeombwa kibali.

Ukibatilisha (kughairi) idhini yako ya elimu yote maalum na huduma zinazohusiana kwa kuandika wakati wowote baada ya mtoto wako kwanza kupata elimu maalum na huduma zinazohusiana, wilaya ya shule haipaswi kuendelea kutoa huduma hizo, lakini inaweza ikakupa taarifa iliyoandikwa, kama ilivyoelezwa chini ya mada ***Taarifa ya Awali kwa Maandishi***, kabla ya kuacha kutoa huduma hizo.

**Kibali cha mzazi kuhusu tathmini mpya**

Wilaya yako ya shule lazima ipate kibali chako kabla kumtathmini tena mtoto wako, isipokuwa kama wilaya yako ya shule inaweza kuonyesha kwamba:

1. Imechukua hatua stahiki ya kupata kibali chako ili kumtathmini upyaji mtoto wako; **na**

2. Hukujibu.

Ukikataa kukubali mtoto wako afanyiwe tathmini upya, wilaya ya shule inaweza, lakini si lazima, kufuatilia tathmini mpya ya mtoto wako kwa kutumia usuluhishi, malalamiko yanayofuata mchakato, mkutano wa utatuzi na kusikilizwa katika mchako huria ili kutaka kutengua hatua yako ya kukataa kutoa kibali ili mtoto wako uhakikiwe upya. Kama ilivyo kwa tathmini za awali, wilaya yako ya shule haivunyi majukumu yake chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA ikikataa kufuatilia tathmini mpya kwa njia hii.

**Uandikaji wa nyaraka kuhusu juhudi za kutafuta kibali cha mzazi**

Shule yako sharti ihifadhi nyaraka za jitihada za kutosha za kutaka kupata kibali chako cha tathmini za mwanzo, ili kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, kwa ajili ya tathmini mpya, na kupata wazazi wa watoto wa Serikali kwa ajili ya tathmini ya awali. Nyaraka lazima zijumuishe rekodi ya majaribio ya wilaya ya shule katika masuala kama vile:

1. Rekodi za simu zilizopigwa au kujaribiwa na matokeo ya simu hizo;

2. Nakala za mawasiliano zilizotumwa kwako na majibu yoyote yaliyopokelewa; **na**

3. Kumbukumbu za kina za kutembelea nyumbani kwako au mahali pa kazi na matokeo ya utembeleaji huo.

**Mahitaji mengine ya kibali**

Ruhusa yako haihitajiki kabla wilaya yako ya shule iweze:

1. Kukagua data zilizopo kama sehemu ya tathmini ya mtoto wako au tathmini mpya; **au**

2. Kumpa mtoto wako mtihani au tathmini nyingine ambayo hutolewa kwa watoto wote isipokuwa, kabla ya mtihani huo au tathmini, idhini inahitajika kutoka kwa wazazi wa watoto wote.

Ikiwa umemsajili mtoto wako katika shule binafsi kwa gharama yako mwenyewe au ikiwa unamfundisha mtoto wako nyumbani na hujatoa kibali chako kwa tathmini ya awali ya mtoto wako au tathmini mpya ya

mtoto wako, au hukujibu ombi la kutoa kibali chako, wilaya ya shule haiwezi kutumia taratibu zake za kutatua migogoro (yana ni, usuluhishi, malalamiko yanayofuata mchakato, mkutano wa utatuzi, au kusikilizwa katika mchako huria) na haipaswi kuchunguza kama mtoto wako anastahiki kupata huduma zinazofaa (huduma zinazopatikana kwa baadhi ya watoto walio katika shule walizochaguliwa na wazazi wao lakini ni wenye ulemavu).

## *KIBALI CHA MZAZI KWA MABADILIKO YA MIHIMU KATIKA HUDUMA AU MABADILIKO MAKUBWA YANAYOHUSU MAHALI MTOTO ANAPOSOMA

**K.S.A. 72-988(b)(6), K.S.A. 72-962(aa), K.S.A. 72-962(bb), K.A.R. 91-40-27(a)(3), K.A.R. 91-40-1(mm), and 91-40-1(sss)**

Wilaya ya shule inapaswa kupata kibali cha mzazi kwa maandishi kabla ya kufanya "mabadiliko muhimu katika huduma" au "mabadiliko makubwa yanayohusu mahali mtoto anaposoma." Mabadiliko muhimu katika huduma ni ongezeko au kupungua kwa asilimia 25 au zaidi kwa muda au mzunguko wa huduma maalum ya elimu, huduma inayohusiana au usaidizi au huduma ya ziada inayoelezwa kwenye IEP ya mtoto aliye na mahitaji ya kipekee. Mabadiliko makubwa yanahusu kubadilisha mahali mtoto mwenye mahitaji ya kipekee anaposoma, kwa zaidi ya asilimia 25 ya siku za shule kwa mtoto, kutoka mazingira yasiyo na udhibiti mkubwa hadi katika mazingira yaliyo na udhibiti mkubwa au kutoka mazingira yaliyo na udhibiti mkubwa hadi mazingira yaliyo na udhibiti mdogo.

## *KUBATILISHA KIBALI KWA HUDUMA MAHUSUSI

**K.A.R. 91-40-1(l)(3)(C) and K.A.R. 91-40-27(k)**

Wazazi wana haki ya kubatilisha kibali kwa huduma fulani au mahali mtoto anaposoma ikiwa timu ya IEP itathibitisha kwa kuandika kwamba mtoto hana haja ya huduma au masomo ambayo idhini yake inafutiliwa ili kupata elimu ya umma inayofaa.

## TATHMINI HURU YA MAHITAJI YA KIELIMU

**34 CFR §300.502**

**Kwa Ujumla**

Kama inavyoelezwa hapa chini, una haki ya kupata tathmini huru ya mahitaji ya kielimu ya mtoto wako (IEE) ikiwa hukubaliana na tathmini ya mtoto wako ambayo ilitolewa na wilaya yako ya shule.

Ukiomba tathmini huru ya mahitaji ya kielimu ya mtoto, wilaya ya shule lazima ikupe taarifa kuhusu wapi unaweza kupata tathmini huru ya mahitaji ya kielimu na vigezo vya wilaya ya shule ambavyo vinahusu tathmini huru za kielimu.

**Fasili**

*Tathmini huru ya mahitaji ya kielimu* inamaanisha tathmini inayofanywa na mchunguzi aliyehitimu ambaye si mwajiri wa wilaya ya shule inayohusika na elimu ya mtoto wako.

*Malipo ya umma* inamaanisha kuwa wilaya ya shule hulipa gharama kamili ya tathmini au huhakikisha kwamba tathmini hiyo haikusababishii gharama yoyote, kulingana na masharti ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA. Kufanya hivyo huruhusu kila Jimbo kutumia kila rasilimali iwe ya Jimbo, mtaa, Taifa, na vyanzo binafsi ambavyo vinapatikana katika Jimbo kukidhi mahitaji ya Sehemu B ya Sheria.

**Haki ya kutathminiwa kwa gharama ya umma**

Una haki ya una haki ya kupata tathmini huru ya mahitaji ya kielimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma ikiwa hukubaliani na tathmini ya mtoto wako iliyofanywa na wilaya yako ya shule, ilimradi yafuatayo yatimizwe:

1. Ukiomba tathmini huru ya mahitaji ya kielimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma, wilaya yako ya shule lazima, bila kuchelewa pasipo sababu, inafaa : (a) Kuanzisha malalamiko yanayofuata mchakato ili iombe kusikilizwa kwa lengo la kuonyesha kwamba tathmini iliyofanyia mtoto wako ni sahihi; au (b) Ifanye tathmini huru ya mahitaji ya kielimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma, isipokuwa kama wilaya ya shule imethibitisha wakati wa kusikilizwa kwamba tathmini uliyomtafutia mtoto wako haikutimiza vigezo vya wilaya ya shule.

2. Ikiwa wilaya yako ya shule itaomba kusikilizwa na uamuzi wa mwisho uwe kwamba tathmini ya wilaya yako ya shule ni sahihi, bado una haki ya kufanya tathmini huru ya mahitaji ya kielimu ya mtoto wako, lakini si kwa gharama ya umma.

3. Ukiomba tathmini huru ya mahitaji ya kielimu ya mtoto wako, wilaya ya shule inaweza kukuuliza kwa nini unakataa tathmini ya mtoto wako uliyofanywa na wilaya yako ya shule. Hata

hivyo, wilaya yako ya shule huenda isihitaji maelezo na haiweza kuchelewesha tathmini huru ya mahitaji ya kielimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma au kuanzisha malalamiko yanayofuata mchakato ili kuomba isikilizwe kuhusiana na utetezi ulio nao kuhusi jinsi wilaya ya shule ilivyomtathmini mtoto wako.

Unakibali cha kupata tathmini moja pekee huru ya mahitaji ya kielimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma kila wakati wilaya yako ya shule inapofanya tathmini ya mtoto wako ambayo hukubaliani nayo.

**Tathmini zinazoanzishwa na mzazi**

Ukupata tathmini huru ya mahitaji ya kielimu ya mtoto wako kwa gharama za umma au uipatie wilaya ya shule tathmini ya mtoto wako uliyopata kwa gharama binafsi:

1. Wilaya yako ya shule inapaswa kuzingatia matokeo ya tathmini ya mtoto wako, ikiwa inatimiza vigezo vya wilaya ya shule vinavyosimamia tathmini huru ya mahitaji ya kielimu katika uamuzi wowote unaofanywa kuhusiana na utoaji wa elimu inayofaa ya umma bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako; **na**

2. Wewe au wilaya yako ya shule inaweza kuwasilisha tathmini kama ushahidi wakati wa kikao cha kusikilizwa kinachohusiana na mtoto wako.

**Maombi ya tathmini yanayofanywa na maofisa wanaosikiliza**

Ofisa anayesikiliza suala linalohusu mtoto wako anaweza akaomba tathmini huru ya mahitaji ya kielimu ya mtoto wako kama sehemu ya mchakato wa usikilizaji, gharama ya tathmini lazima iwe kwa umma.

**Vigezo vya wilaya ya shule**

Ikiwa tathmini huru ya mahitaji ya kielimu ni kwa gharama ya umma, vigezo vya tathmini, ikiwa ni pamoja na eneo la tathmini na sifa za mchunguzi, lazima viwe sawa na vigezo ambavyo wilaya ya shule hutumia wakati inapofanya tathmini (ilimradi vigezo hivi viwe vinatii haki yako ya tathmini huru ya mahitaji ya kielimu).

Isipokuwa kwa kuzingatia vigezo vilivyoelezwa hapo juu, wilaya ya shule haipaswi kulazimishia hali au ratiba za kupata tathmini ya huru ya kielimu kwa gharama ya umma.

# USIRI WA TAARIFA

## FASILI

**34 CFR §300.611**

Jinsi inavyotumiwa chini ya mada Usiri wa Taarifa:

- *Kuharibu* kunamaanisha kuharibu umbo au uondoaji wa sifa zinazoweza kumtambulisha mtu binasfi ili taarifa zisiweze kuhusishwa na mtu tena.
- *Rekodi za elimu* inamaanisha aina ya rekodi zinazotajwa chini ya ufafanuzi wa ‘‘rekodi za elimu’’' katika kifungu cha 34 CFR Sehemu ya 99 (kanuni za kutekeleza Sheria ya Haki na Faragha ya Familia katika Elimu ya 1974, 20 USC 1232g (FERPA)).
- *Shirika linalohusika* inamaanisha wilaya yoyote, wakala au taasisi ambayo inakusanya, inaweka, au kutumia taarifa binafsi ambazo zinazotambulika, au ambazo zinatoa taarifa kwa mujibu wa Sehemu ya B ya sheria ya IDEA.

## SIFA TAMBULISHI

**34 CFR §300.32**

*Sifa tambulishi* inarejelea taarifa zinazojumuisha:

(a) Jina la mtoto wako, jina lako mzazi, au jina la ndugu mwingine katika familia;

(b) Anwani ya mtoto wako;

(c) Kitambulisho cha binafsi, kama vile namba ya usalama wa jamii ya mtoto wako au namba ya shule; **au**

(d) Orodha ya sifa binafsi au taarifa nyingine ambazo zinaweza kumtambulisha mtoto wako kwa hakika.

## TAARIFA KWA WAZAZI

**34 CFR §300.612**

Idara ya Elimu Jimboni inapaswa kutoa taarifa inayotosha kuwajulisha wazazi kuhusu usiri wa taarifa za binafsi zinazoweza kutambulisha, ikiwa ni pamoja na:

1. Maelezo ya kiwango ambacho taarifa hiyo inatolewa katika lugha za asili za makundi mbalimbali ya watu katika Jimbo;
2. Maelezo kuhusu watoto ambao taarifa zao za binafsi zinazotambulika zinahifadhiwa, aina ya taarifa zinazotakiwa, mbinu ambazo Jimbo linakusudia kutumia katika kukusanya taarifa (ikiwa ni pamoja na vyanzo vya kutoa taarifa), na jinsi taarifa zitakavyotumiwa;
3. Muhtasari wa sera na taratibu ambazo mashirika yanayohusika lazima yafuate katika kuhifadhi, kutoa taarifa kwa watu wengine, kubakiza, na kuharibu taarifa za binafsi; **na**
4. Maelezo ya haki zote za wazazi na watoto kuhusu taarifa hii, ikiwa ni pamoja na haki chini ya Sheria ya Haki na Faragha ya Familia katika Elimu (FERPA) na kanuni zake za utekelezaji katika 34 CFR Sehemu ya 99.

Kabla ya shughuli yoyote kuu kutambua, kupata, au kutathmini watoto wanaohitaji elimu maalum na huduma zinazohusiana (pia inajulikana kama "kumpata mtoto"), taarifa hiyo inapaswa kuchapishwa au kutangazwa katika magazeti au vyombo vingine vya habari, au vyote, vinavyosambaza vizuri ili kuwaarifu wazazi katika Jimbo kuhusu shughuli hizi.

## HAKI ZA KUPATA

**34 CFR §300.613**

Shirika linalohusika lazima likuruhusu ukague na kuchunguza kumbukumbu yoyote ya elimu inayohusiana na mtoto wako ambayo inakusanywa, kuhifadhiwa, au kutumiwa na wilaya yako ya shule chini ya Sehemu B ya sheria ya IDEA. Shirika linalohusika linapaswa kuzingatia ombi lako ili kukagua na kurekebisha rekodi yoyote ya elimu inayomhusu mtoto wako bila kuchelewa na kabla ya mkutano wowote unaohusu mpango mahususi kwa elimu ya mtoto (IEP), au utaratibu wowote mchakato wa kusikilizwa

(ikiwa ni pamoja na mkutano wa kutafuta suluhu au kikao cha nidhamu), na isipite zaidi ya siku 45 za kalenda baada ya ombi lako.

Haki yako ya kupitia na kukagua kumbukumbu za elimu inajumuisha:

1. Haki yako ya kujibiwa na shirika husika unapoomba kwa uzuri upewe maelezo na ufafanuzi wa rekodi;

2. Haki yako ya kuomba mashirika yanayohusika yakupe nakala za rekodi ikiwa huwezi kuchunguza kwa ufanisi na kukagua rekodi bila kupokea nakala hizo; **na**

3. Haki yako ya mwakilishi wako kuruhusiwa ahakike na kukagua rekodi.

Shirika linalohusika linaweza kuchukulia kuwa una mamlaka ya kupitia na kukagua rekodi zinazohusiana na mtoto wako isipokuwa ishauriwe kuwa huna mamlaka chini ya sheria husika ya Jimbo inayosimamia mambo kama vile utunzaji, kutengana, na talaka.

## KUFIKIA REKODI

**34 CFR §300.614**

Kila taasisi inayohusika lazima iweke rekodi ya watu wanaoruhusiwa kufikia rekodi za elimu zilizokusanywa, kuhifadhiwa, au kutumika chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA (isipokuwa uwe ufikiaji unaofanywa na wazazi na wafanyakazi walioruhusiwa na shirika husika), ikiwa ni pamoja na jina la mhusika, tarehe ambapo idhini ya kufikia ilitolewa, na kusudi ambalo lilifanya mhusika aruhusiwe kutumia rekodi.

## REKODI ZA ZAIDI YA MTOTO MMOJA

**34 CFR §300.615**

Ikiwa rekodi yoyote ya elimu ina taarifa kuhusu mtoto zaidi ya moja, wazazi wa watoto hao wana haki ya kupitia na kukagua taarifa zinazohusiana na mtoto wao pekee au kujulishwa kuhusu taarifa hizo pekee.

## ORODHA YA AINA NA SEHEMU TAARIFA ZILIPO

**34 CFR §300.616**

Unapoomba, kila taasisi inayohusika inapaswa kukupa orodha ya aina na maeneo ya rekodi za elimu zilizokusanywa, kuhifadhiwa, au kutumika na shirika hilo.

## ADA

**34 CFR §300.617**

Kila taasisi inayohusika inaweza ikakutoza ada kwa nakala za rekodi ambazo unafanyiwa kwa mujibu wa Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, ikiwa ada haikuzuiei haki yako ya kupitia na kukagua rekodi hizo.

Shirika linalohusika haliwezi kutoza ada ya kutafuta au kupata taarifa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA.

## MAREKEBISHO YA KUMBUKUMBU KWA OMBI LA MZAZI

**34 CFR §300.618**

Ikiwa unaamini kuwa taarifa zilizo katika rekodi za elimu kuhusu mtoto wako zilizokusanywa, kuhifadhiwa, au kutumika chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA si sahihi, inapotosha, au inakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, unaweza kuomba shirika linalohusika lililo na taarifa hizo kuzibadilisha.

Shirika linalohusika linapaswa kuamua kama linafaa kubadilisha taarifa hizo kwa mujibu wa ombi lako ndani ya muda unaofaa baada ya kupokea ombi lako.

Ikiwa shirika linalohusika litakataa kubadili taarifa kulingana na ombi lako, ni lazima likujulishe kuhusu kukataa huko na kukushauri kuhusu haki uliyo nayo kusikilizwa jinsi ilivyoelezwa chini ya mada ya ***Fursa ya Kusikilizwa***.

## FURSA YA KUSIKILIZWA

**34 CFR §300.619**

Baada ya kuomba, shirika linalohusika linapaswa likupe fursa ya kusikilizwa ili ukosoe taarifa zilizo katika rekodi za elimu za mtoto wako ili kuhakikisha kuwa ni sahihi, haipotoshi, au kukiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako.

## UTARATIBU WA KUSIKILIZWA

**34 CFR §300.621**

Kikoa cha kusikilizwa ili kukosoa rekodi za elimu lazima kifanyike kulingana na taratibu zilizo kwenye Sheria ya Haki na Faragha ya Familia katika Elimu (FERPA).

## MATOKEO YA KUSIKILIZWA

**34 CFR §300.620**

Ikiwa baada ya kusikilizwa, shirika husika litaamua kuwa taarifa si sahihi, inapotosha au kwa namna nyingineyo inakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, ni lazima ibadilishe taarifa kwa usahihi na kukujulisha kwa maandishi.

Ikiwa baada ya kusikiliza, shirika husika litaamua kwamba taarifa ni sahihi, haipotoshi, au kukiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, ni lazima likujulishe haki uliyo nayo ya kujumuisha katika kumbukumbu ambazo inashikilia za mtoto wako, taarifa iliyo na msimamo wako kuhusu taarifa hizo au utoe sababu yoyote ambayo inafanya usikubaliane na uamuzi wa shirika husika.

Maelezo kama hayo yatakayowekwa katika kumbukumbu za mtoto wako lazima:

1. Yahifadhiwe na shirika husika kama sehemu ya kumbukumbu za mtoto wako katika kipindi chote cha kumbukumbu au kipindi chote ambapo sehemu inayopingwa inaendelea kuhifadhiwa na shirika husika; **na**

2. Yajumuishwe katika kumbukumbu za mtoto wako ikiwa shirika husika litafichua kumbukumnbu za mtoto wako au taarifa zinazopingwa kwa mtu mwingine yeyote.

## RUHUSA YA KUFICHUA TAARIFA ZA SIFA TAMBULISHI

**34 CFR §300.622**

Isipokuwa kama maelezo yapo kwenye rekodi za elimu, na ufichuaji unaidhinishwa bila kibali cha mzazi chini ya Sheria ya Haki na Faragha ya Familia katika Elimu (FERPA), unafaa kuombwa kibali kabla taarifa binafsi inayoweza kutambulishwa ifichuliwe kwa watu wengine wasio maofisa wa mashirika husika. Isipokuwa chini ya mazingira yaliyotajwa hapa chini, si sharti utoe kibali kabla ya taarifa binafsi inayoweza kutambulishwa itolewa kwa maofisa wa mashirika husika kwa madhumuni ya kukidhi mahitaji ya Sehemu B ya sheria ya IDEA.

Ruhusa yako, au idhini ya mtoto ambaye amefikia umri wa utu uzima chini ya sheria ya Nchi, inatakiwa kabla ya taarifa binafsi zisizoweza kutambulisha kukabidhiwa kwa maofisa wa mashirika husika yanayotoa au kulipia huduma za mpito.

Ikiwa mtoto wako yuko, au ataenda shule binafsi ambayo haipo katika wilaya ya shule unapoishi, ni lazima utoe kibali kabla ya taarifa yoyote ya binafsi inayoweza kumtambulisha mtoto wako ibadilishwe miongoni mwa maofisa wa wilaya ya shule za umma na wale wa wilaya ambapo shule binafsi ambako mtoto wako anapoenda ipo.

## ULINZI

**34 CFR §300.623**

Kila taasisi inayohusika ni sharti ilinde usiri wa taarifa binafsi zinazoweza kutambulisha katika hatua za kukusanya, kuhifadhi, kufichua na kuharibu.

Ofisa mmoja katika kila taasisi husika anatakiwa achukue jukumu la kuhakikisha usiri wa taarifa yoyote inayoweza kutambulisha.

Watu wote wanaokusanya au kutumia taarifa binafsi zinzoweza kutambulisha wanafaa kufundishwa au kuelekezwa kuhusu sera na taratibu za Serikali kuhusu usiri chini ya Sehemu B ya sheria ya IDEA na Sheria ya Haki na Faragha ya Familia katika Elimu (FERPA).

Kila taasisi husika inapaswa kudumisha orodha ya sasa ya majina na nafasi za wafanyakazi wake ambao wanaweza kufikia taarifa binafsi, kwa ajili ya ukaguzi wa umma.

## KUHARIBU TAARIFA

**34 CFR §300.624**

Wilaya yako ya shule inapaswa kukujulisha wakati taarifa za binafsi zinazoweza kutambulisha ilizokusanya, kuhifadhi, au kutumia chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA hazihitajiki tena kutoa huduma za elimu kwa mtoto wako.

Taarifa lazima ziharibiwe kwa ombi lako. Hata hivyo, kumbukumbu ya kudumu ya jina la mtoto, anwani, namba ya simu, darasa lake, rekodi ya mahudhurio, masomo aliyohudhuria, ngazi akipomalizia na mwaka alipomaliza inaweza kuhifadhiwa bila ya kikwazo cha muda.

# UTARATIBU WA MALALAMIKO YA SERIKALI

## TOFAUTI KATI YA UTARATIBU WA MALALAMIKO NA KUSIKILIZWA KWA KUFUATA MCHAKATO NA MALALAMIKO YA SERIKALI

Kanuni zilizo katika Sehemu ya B ya sheria ya IDEA zinaweka taratibu tofauti za malalamiko ya Serikali na malalamiko ya kusikilizwa kwa kufuata mchakato. Kama ilivyoelezwa hapa chini, mtu yeyote au shirika linaweza kuwasilsiha malalamiko ya Serikali kuhusu ukiukaji wa mahitaji yoyote ya Sehemu ya B unaofanywa na wilaya ya shule, Idara ya Elimu Jimboni, au shirika lolote la umma. Ni wewe tu au wilaya ya shule inyonaweza kufungua malalamiko ya kusikilizwa kwa kufuata mchakato juu ya jambo lolote linalohusiana na pendekezo au kukataa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini, au elimu ya mtoto mwenye ulemavu, au utoaji wa elimu inayofaa ya umma bila malipo (FAPE) kwa mtoto. Ingawa wafanyakazi wa Idara ya Elimu Jimboni kwa ujumla wanapaswa kutatua malalamiko ya Kiserikali ndani ya siku 60 za kalenda, isipokuwa yaongezwe, ofisa asiyeegemea upande wowote lazima asikilize malalamiko yanayofuata mchakato (ikiwa haikutatuliwa kupitia mkutano wa usuluhishi au kwa njia ya upatanisho) na atoe uamuzi ulioandikwa ndani ya siku 45 za kalenda baada ya mwisho wa kipindi cha utatuzi, kama ilivyoelezwa katika hati hii chini ya mada Mchakato wa Utatuzi, isipokuwa ofisa aliyesikia suala aongeze muda maalum kufuatia ombi la wilaya ya shule. Malalamiko ya Kiserikali na malalamiko yanayofuata mchakato, taratibu za usuluhishi na kusikiliza zinaelezwa kikamilifu hapa chini. Idara ya Elimu la Jimboni lazima iandae fomu za mfano ili kukusaidia uwasilishe malalamiko ya mchakato yanayofuata mchakato na kukusaidia au watu wengine kuwasilisha malalamiko ya Kiserikali kama inavyoelezwa chini ya ***Fomu za Mfano***.

## KUKUBALIWA KWA UTARATIBU WA MALALAMIKO YA KISERIKALI

**34 CFR §300.151**

**Kwa Ujumla**

Kila Idara ya Elimu Jimboni lazima iwe na taratibu zilizoandikwa za:

1. Kutatua malalamiko yoyote, ikiwa ni pamoja na malalamiko yanayotolewa na shirika au mtu binafsi kutoka kwa Jimbo jingine;
2. Kuwasilisha malalamiko kwa Idara ya Elimu Jimboni;
3. Kueneza kwa kiasi kikubwa utaratibu wa kufanya malalamiko ya Kiserikali kwa wazazi na watu wengine wenye nia, ikiwa ni pamoja na vituo vya mafunzo na habari kwa wazazi, mashirika ya ulinzi na uhamasishaji, vituo huru vya kusaidiana, na asasi nyingine stahiki.

**Suluhu za kukosa huduma zinazofaa**

Katika kutatua malalamiko ya Kiserikali ambapo Idara ya Elimu Jimboni imegundua mapungufu katika kutoa huduma zinazofaa, Idara ya Elimu Jimboni lazima izingatie yafuatayo:

1. Kushindwa kutoa huduma zinazofaa, ikiwa ni pamoja na hatua za kurekebisha zinazofaa kushughulikia mahitaji ya mtoto (kama vile huduma za kufidia au malipo ya fedha); **<u>na</u>**
2. Utoaji wa huduma bora kwa watoto wote wenye ulemavu siku zijazo.

## KIMA CHA CHINI KWA UTARATIBU WA MALALAMIKO YA KISERIKALI

**34 CFR §300.152**

**Kima cha muda; taratibu zisizofaa kupunguzwa**

Kila Idara ya Elimu Jimboni lazima lijumuishe katika taratibu zake za malalamiko ya Kiserikali kipindi cha siku 60 za kalenda baada ya malalamiko kuwasilishwa ili:

1. Ifanye uchunguzi wake huru katika eneo mahususi, ikiwa Idara ya Elimu Jimboni itaona ni muhimu kufanya uchunguzi huo;
2. Kumpa mlalamikaji nafasi ya kuwasilisha maelezo ya ziada, ama kwa maneno au kwa maandishi, kuhusu madai katika malalamiko;
3. Kuipa wilaya ya shule au shirika jingine la umma fursa ya kujibu malalamiko, ikiwa ni pamoja na, kwa kiwango cha chini: (a) chaguo la shirika kupendekeza kutatua malalamiko; **<u>na</u>** (b) fursa kwa mzazi ambaye ametoa malalamiko na shirika husika kukubaliana kwa hiari kushiriki kupata suluhisho;

4. Kukagua taarifa zote muhimu na kufanya uamuzi huria ikiwa wilaya ya shule au shirika jingine la umma linakiuka matakwa ya Sehemu B ya sheria ya IDEA; **na**

5. Kutoa uamuzi ulioandikwa kwa mlalamikaji unaoshughulikia kila dai katika malalamiko na ina: (a) matokeo ya ukweli na uamuzi; **na** (b) sababu za Idara ya Elimu Jimboni kufanya uamuzi wake.

**Kuongeza muda; uamuzi wa mwisho; utekelezaji**

Taratibu za Idara ya Elimu Jimboni zilizoelezwa hapo juu lazima pia:

1. Ziruhusu kuongeza kipindi cha siku 60 za kalenda ikiwa: (a) kuna hali za kipekee zinazofaa kuzingatiwa katika malalamiko fulani ya Kiserikali; **au** (b) wewe na wilaya ya shule au shirika jingine la umma husika mmekubaliana kwa hiari kuongeza muda ili kutatua suala hilo kwa njia ya upatanisho au njia mbadala ya ufumbuzi wa migogoro, ikiwa inapatikana katika Jimbo.

2. Ijumuishe taratibu bora za utekelezaji wa uamuzi wa mwisho wa Idara ya Elimu, ikiwa inahitajika na ijumuishe: (a) usaidizi wa kiufundi; (b) majadiliano; **na** (c) vitendo vya kurekebisha ili kufikia hali inayotakiwa.

**Kisikilizwa kwa malalamiko ya kiserikali na yanayofuata mchakato**

Malalamiko ya Kiserikali yaliyoandikwa yakipokelewa na yawe sawa na suala la linalosikilizwa kwa kufuata mchakato kama ilivyoelezwa chini ya mada ***Kuwasilisha Malalamiko Yanayofuata Mchakato*** , au ikiwa malalamiko ya Kiserikali yana masuala mengi ambayo mojawapo ni kinachosikilizwa, Jimbo lazima lisiguse sehemu ya malalamiko ya Kiserikali ambayo yanashughulikiwa katika malalamiko yanayofuata mchakato hadi suala hilo litakaposikilizwa. Suala lolote katika malalamiko ya Kiserikali ambalo si sehemu ya kusikilizwa kwa kufuata mchakato ni lazima litatuliwe kwa kutumia muda na taratibu zilizoelezwa hapo juu.

Ikiwa suala linalofufuliwa katika malalamiko ya Kiserikali lilikuwa limeshughulikiwa hapo awali katika malalamiko yanayofuata mchakato kwa wahusika walewale (kwa mfano, wewe na wilaya ya shule), basi uamuzi wa malalamiko yanayofuata mchakato utadumishwa katika suala hilo na Idara ya Elimu Jimboni linapaswa kumwambia mlalamikaji kwamba uamuzi huo hauwezi kubadilishwa.

Malalamiko yanayodai kwamba wilaya ya shule au shirika jingine la umma limeshindwa kutekeleza uamuzi uliotolewa katika malalamiko yanayofuata mchakato ni lazima usuluhishwe na Idara ya Elimu Jimboni.

## KUWASILISHA MALALAMIKO YA KISERIKALI

**34 CFR §300.153**

Shirika au mtu binafsi anaweza kuwasilisha malalamiko ya Kiserikali kwa kufuata taratibu zilizoelezwa hapo juu.

Malalamiko ya Kiserikali lazima yawe na yafuatayo:

1. Taarifa kwamba wilaya ya shule au shirika jingine la umma limekiuka matakwa ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA au kanuni zake za utekelezaji katika 34 CFR Sehemu ya 300;

2. Ukweli ambao ambao umesababisha malalmiko kuwasilsihwa;

3. Saini na anwani ya mawasiliano ya mlalamikaji; na

4. Ikiwa madai ya ukiukwaji yanmhusu mtoto mahususi:

(a) Jina la mtoto na anwani ya makazi ya mtoto;

(b) Jina la shule ambalo mtoto anasoma;

(c) Katika hali abapo mtoto au kijana hana makazi, anwani iliyopo ya mtoto na jina la shule ambapo mtoto anasoma;

(d) Maelezo ya hali ya tatizo la mtoto, ikiwa ni pamoja na ufafanuzi kuhusiana na tatizo; **na**

(e) Pendekezo la kutatua tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kinachopatikana kwa upande wa mlalamikaji wakati wa kuwasilisha malalamiko.

Malalamiko lazima yawe ya madai yaliyotokea kipindi kisichozidi mwaka mmoja kabla ya tarehe ambayo malalamiko yanapokelewa kama ilivyoelezwa chini ya ***Taratibu za Kupokea Malalamiko ya Kiserikali.***

Upande unaowasilisha malalamiko ya Kiserikali lazima uwasilishe nakala ya malalamiko kwa wilaya ya shule au shirika jingine la umma linamtumikia mtoto wakati ambapo anawasilisha malalamiko kwa Idara ya Elimu Jimboni.

# UTARATIBU WA MALALAMIKO YANAYOFUATA MCHAKATO

## KUWASILISHA MALALAMIKO YANAYOFUATA MCHAKATO

**34 CFR §300.507**

**Kwa Ujumla**

Ni wewe tu au wilaya ya shule inyonaweza kufungua malalamiko ya kusikilizwa kwa kufuata mchakato juu ya jambo lolote linalohusiana na pendekezo au kukataa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini, au elimu ya mtoto mwenye ulemavu, au utoaji wa elimu inayofaa ya umma bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako.

Malalamiko yanayofuata mchakato lazima yahusu madai ya ukiukwaji uliotokea kipindi kisichozidi miaka miwili kabla wewe au wilaya ya shule ujue juu kuhusu tukio linalodaiwa linafaa kuanzishiwa malalamiko yanayofuata mchakato.

Muda ulio hapa juu hatakubana ikiwa hukuweza kuwasilisha malalamiko yanayofuata mchakato katika kipindi hicho kwa sababu:

1. Wilaya ya shule ilikosea kwa kudhani kwamba ilikuwa imetatua masuala unayotaja katika malalamiko; **au**

2. Wilaya ya shule haikukupa taarifa ilizofaa kukupatia kwa mujibu wa Sehemu ya B ya sheria ya IDEA.

**Taarifa kwa ajili ya wazazi**

Wilaya ya shule inapaswa kukujulisha huduma za kisheria za bure au za gharama nafuu na huduma nyingine zinazohusiana na suala unaloomba taarifa kuhusu, **au** ikiwa wewe au wilaya ya shule mnawasilisha malalamiko yanayofuata mchakato.

## MALALAMIKO YANAYOFUATA MCHAKATO

**34 CFR §300.508**

**Kwa Ujumla**

Ili kuomba kusikilizwa, wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule) lazima uwasilishe malalamiko yanayofuata mchakato kwa upande mwingine husika. Malalamiko hayo lazima yawe na maudhui yote yaliyoorodheshwa hapa chini na sharti kuwekwa siri.

Yeyote anayewasilisha malalamiko lazima pia aipe Idara ya Elimu Jimboni nakala ya malalamiko.

**Maudhui ya malalamiko**

Malalamiko yanayofuata mchakato lazima yawe na:

1. Jina la mtoto;

2. Anwani ya makazi ya mtoto;

3. Jina la shule ya mtoto;

4. Ikiwa ni mtoto au kijana asiye na kwao, anwani ya mawasiliano ya mtoto na jina la shule ya mtoto;

5. Maelezo ya aina ya tatizo la mtoto linavyohusiana na hatua inayopendekezwa au iliyokataliwa, ikiwa ni pamoja na ufafanuzi kuhusiana na tatizo; **na**

6. Pendekezo la kutatua tatizo kwa kiwango kinachojulikana na kinachopatikana kwa upande unaolalamika (wewe au wilaya ya shule) wakati huo.

**Ilani inayotakiwa kabla ya malalamiko yanayofuata mchakato**

Wewe au wilaya ya shule hampaswi kuwa na kikao cha kusikilizwa kwa kufuata mchakato hadi wewe au wilaya ya shule (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule) mwasilishe malalamiko yanayofuata mchakato yanajumuisha maelezo yaliyotajwa hapo juu.

**Utoshelevu wa malalamiko**

Ili malalamiko yanayofuata mchakato yaendelee, lazima yachukuliwe kuwa na utoshelevu. Malalamiko yanayofuata mchakato yatachukuliwa kuwa na utoshelevu (kutimiza masharti ya maudhui yaliyotajwa

hapo juu) isipokuwa upande mwingine wa malalamiko yanayofuata mchakato (wewe au wilaya ya shule) umjulishe ofisa wa kusikiliza na upande mwingine husika kwa maandishi ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea malalamiko, kwamba upande uliopokea unaamini kwamba malalamiko yanayofuata mchakato haujatimiza masharti yaliyoorodheshwa hapo juu.

Ndani ya siku tano za kalenda tangu kupokea taarifa kwamba upande uliopokea malalamiko (wewe au wilaya ya shule) unaona kuwa malalamiko yanayofuata mchakato hautoshelezi, ofisa anayesikiliza lazima aamua kama malalamiko yayofuata mchakato yanakidhi mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu, na kukuarifu wewe na wilaya ya shule kwa maandishi mara moja.

**Kurekebisha malalamiko**

Wewe au wilaya ya shule inaweza tu kurekebisha malalamiko ikiwa:

1. Upande mwingine husika utakubali mabadiliko kwa kuandika na unapewa fursa ya kutatua malalamiko yanayofuata mchakato kupitia mkutano wa utatuzi, ulivyoelezwa chini ya ***Mchakato wa Utatuzi*** ; **au**

2. Katika kipindi kisichopungua siku tano kabla ya vikao vya kusikia malalamiko yanayofuata mchakato, ofisa husika atoe ruhusa ya kufanya mabadiliko.

Ikiwa upande unaolalamika (wewe au wilaya ya shule) utafanya mabadiliko kwa malalamiko yanayofuata mchakato, kipindi cha mkutano wa utatuzi (ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea malalamiko) na kipindi cha utatuzi (ndani ya siku 30 za kalenda baada ya kupokea malalamiko) utaanza kuhesabiwa tena kuanzia tarehe ambapo malalamiko yalirekebishwa.

**Jibu la usimamizi wa elimu katika mtaa (LEA) au wilaya ya shule kwa malalamiko yanayofuata mchakato**

Ikiwa wilaya ya shule haijakutumia taarifa ya awali kwa maandishi, kama ilivyoelezwa chini ya ***Taarifa ya Awali kwa Maandishi***, kuhusu suala lililo katika malalamiko yako yanayofuata mchakato, wilaya ya shule, ndani ya siku 10 za kalenda baada ya kupokea malalamiko ya mchakato, lazima ikutumie jibu linalojumuisha:

1. Maelezo kuhusu kwa nini wilaya ya shule ilipendekeza au ikakataa kuchukua hatua iliyotolewa katika malalamiko yanayofuata mchakato;

2. Maelezo ya chaguo nyingine ambazo Timu ya Mpango Mahususi kwa Elimu ya Mtoto (IEP) imezingatia na sababu za kukataa chaguo hizo;

3. Ufafanuzi wa utaratibu wa kila tathmini, mtihani, rekodi, au taarifa ambazo wilaya ya shule imetumia kuwa msingi wa hatua inayopendekezwa au iliyokataliwa; **na**

4. Ufafanuzi wa mambo mengine ambayo yanafaa kwa hatua ya wilaya ya shule iliyopendekezwa au kukataliwa.

Kutoa taarifa zilizo katika vipengele 1-4 hapo juu havizuii wilaya ya shule kusema kuwa malalamiko yako yanayofuata mchakato hayakutimiza vigezo.

**Majibu upande mwingine kwa malalamiko yanayofuata mchakato**

Isipokuwa kama ilivyoelezwa chini ya kichwa kidogo kinachotangulia, ***Jibu la usimamizi wa elimu katika mtaa ( LEA) aau wilaya ya shule kwa malalamiko yanayofuata mchakato*** , upande unaopokea malalamiko yanayofuata mchakato lazima, ndani ya siku 10 za kalenda baada ya kupokea malalamiko, umtumie upande mwingine husika jibu ambalo linahusu kimahususi masuala yaliyo katika malalamiko.

## FOMU ZA MIFANO

**34 CFR §300.509**

Idara ya Elimu la Jimboni lazima iandae fomu za mfano ili kukusaidia wewe au mtu mwingine uwasilishe malalamiko ya Kiserikali. Hata hivyo, huenda Jimbo lako au wilaya ya shule haitakutaka utumie fomu hizo za mfano. Kwa kweli, unaweza kutumia fomu ya mfano au fomu nyingine inayofaa, ilimradi ina taarifa zinazohitajika kuanzisha malalamiko yanayofuata mchakato au malalamiko ya Kiserikali.

## USULUHISHI

**34 CFR §300.509**

**Kwa Ujumla**

Wilaya ya shule lazima itayarishe taratibu zinazofanya upatanisho uwepo ili kukuruhusu wewe na wilaya ya shule mtatue tofauti zozote za masuala yaliyo chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, yakiwemo mambo yaliyotokea kabla ya kuwasilisha malalamiko yanayofuata mchakato. Kwa hivyo, usuluhishi unaweza kutumiwa kutatua migogoro chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, uwe umewasilisha malalamiko yanayofuata mchakato au la kwa lengo la kuomba kusikilizwa jinsi ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Kuwasilisha Malalamiko Yanayofuata Mchakato***.

**Mahitaji**

Taratibu lazima zihakikishe kwamba mchakato wa usuluhishi:

1. Ni wa hiari kwako na kwa upande wa wilaya ya shule;
2. Hautumiwi kunyima au kuchelewesha haki yako ya kusikilizwa katika mchakato unaofuta hatua, au kukunyima haki nyingine yoyote iliyo chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA; **na**
3. Unaendeshwa na mpatanishi mwenye ujuzi na asiyeegemea upande wowote na ambaye amefundishwa kuhusu mbinu bora za upatanishi.

Wilaya ya shule inaweza ikatayarisha taratibu ambazo zinawapa wazazi na shule ambazo zitaamua kutotumia mchakato wa usuluhishi fursa ya kukutana, kwa wakati na eneo linalokufaa, pamoja na mtu asiye na maslahi katika suala husika:

1. Ambaye ana mkataba na asasi stahiki ya mbinu mbadala za utatuzi wa migogoro, au kituo cha mafunzo na taarifa kwa wazazi au kituo cha rasilimali kwa wazazi katika Jimbo; **na**
2. Ambaye anaweza kukufafanulia na kuhamasisha kuhusu faida za mchakato wa usuluhishi.

Jimbo linapaswa kuwa na orodha ya watu ambao wana sifa ya kuwa wapatanishi na wanaojua sheria na kanuni zinazohusiana na utoaji wa elimu maalum na huduma zinazohusiana. Idara ya Elimu la Jimboni lazima lichague wapatanishi kwa msingi usio na upendeleo, wa mzunguko, au mwingine.

Serikali ya Jimbo litagharimia mchakato wa usuluhishi, ikiwa ni pamoja na gharama za mikutano.

Kila mkutano katika mchakato wa usuluhishi lazima upangwe kwa wakati na ufanyike mahali ambapoo ni muafaka kwako na wilaya ya shule.

Ikiwa wewe na wilaya ya shule mtatatua mgogoro kupitia mchakato wa usuluhishi, mnafaa kuwa na mkataba wa kisheria ambao unaanzisha muafaka huo na:

1. Kusema kuwa majadiliano yote yaliyofanyika wakati wa mchakato wa usuluhishi yataendelea kuwa ya siri na hayatatumiwa kama ushahidi katika kusikia kwa mchakato wowote unaofuata au kesi ya kiraia (shtaka mahakani); **na**
2. Utiwe saini na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye ana mamlaka ya kuiwakilisha wilaya ya shule.

Mkataba wa upatanishi ulioandikwa na kutiwa saini unaweza kutekelezwa katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye mamlaka na uwezo (mahakamani ambayo ina mamlaka chini ya sheria ya Majimbo kusikiliza aina hizo za kesi) au katika mahakama ya wilaya nchini Marekani.

Majadiliano yaliyofanyika wakati wa mchakato wa usuluhishi lazima yawe siri. Hayawezi kutumika kama ushahidi katika kusikilizwa kwa mchakato wakati wowote siku zijazo au katika mashtaka ya kiraia katika mahakama yoyote ya Kitaifa au mahakama ya Jimbo linalopokea msaada chini ya Sehemu B ya sheria ya IDEA.

**Uhuru wa mpatanishi**

Mpatanishi:

1. Hafai kuwa mfanyakazi wa Idara ya Elimu Jimboni au wilaya ya shule ambayo inahusishwa katika elimu au huduma kwa mtoto wako; **na**
2. Lazima asiwe na maslahi ya binafsi au ya kitaaluma ambayo yanaingiliana na mwelekeo wa mpatanishi.

Mtu ambaye ana sifa za kuwa mpatanishi si mfanyakazi wa wilaya ya shule au asasi ya Jimbo kwa sababu analipwa na asasi au wilaya ya shule ili awe mpatanishi.

## MCHAKATO WA UTATUZI

**34 CFR §300.510**

**Mkutano wa utatuzi**

Ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea taarifa ya malalamiko yanayofuata mchakato, kabla ya mchakato wa kusikiliza haujaanza, wilaya ya shule lazima ifanye mkutano na upande/pande husika au Timu ya mpango mahususi kwa elimu ya mtoto (IEP) ambayo ina ujuzi maalum kuhusu masuala yaliyotambuliwa katika malalamiko yako yanayofuata mchakato. Mkutano:

1. Lazima uwe na mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye ana mamlaka ya kufanya maamuzi kwa niaba ya wilaya ya shule; **na**
2. Haufai kuwa na wakili wa wilaya ya shule isipokuwa ikiwa unaongozana na wakili.

Wewe na wilaya ya shule mtaamua wanachama bora wa Timu ya IEP anayefaa kuhudhuria mkutano huo.

Kusudi la mkutano ni kwa wewe kukuruhusu mjadili malalamiko yako yanayofuata mchakato na msingi wa malalamiko, ili wilaya ya shule iwe na nafasi ya kutatua mgogoro huo.

Mkutano wa utatuzi si lazima kama:

1. Wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kwa kuandika ikwamba hakuna haja ya mkutano; **au**
2. Wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kutumia mchakato wa usuluhishi, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Usuluhishi***.

**Kipindi cha utatuzi**

Ikiwa wilaya ya shule itakuwa haijatatulia malalamiko yako yanayofuata mchakato kwa namna inayokuridhisha ndani ya siku 30 za kalenda baada ya kupokea malalamiko yanayofuata mchakato (wakati wa mchakato wa utatuzi), kikao cha mchakato wa kusikilizwa kinaweza kufanyika.

Muda wa siku 45 za kalenda kwa ajili ya kutoa uamuzi wa mwisho wa mchakato, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa, ***Maamuzi ya Kusikilizwa***, huanza mwishoni mwa kipindi cha utatuzi ambacho ni siku 30 za kalenda, kukiwa na tofauti kidogo za marekebisho katika kipindi cha siku 30 za kalenda kwa ajili ya utatuzi, kama ilivyoelezwa hapa chini.

Isipokuwa pale ambapo wewe na wilaya ya shule mmekubaliana kutofanya mchakato wa utatuzi au kutumia upatanisho, kushindwa kushiriki kwenye mkutano wa utatuzi kutachelewesha muda wa mchakato wa utatuzi mchakato wa kusikilizwa mpaka mkutano ufanyike.

Ikiwa baada ya kufanya jitihada za kutosha na kuandika jitihada hizo kwenye kumbukumbu na bado wilaya ya shule ikose kukushawishi kushiriki katika mkutano wa upatanisho, mwisho wa kipindi cha siku 30 za kalenda zinazotumiwa kwa utatuzi, wilaya ya shule inaweza kumwombi ofisa husika atupilie mbali malalamiko yako yanayofuata mchakato. Kumbukumbu ya jitihada hizo lazima zijumuishe rekodi ya majaribio ya wilaya ya shule kuweka mpango wa muda na mahali ambapo panaweza kuwafaa nyote, kama vile:

1. Rekodi za simu zilizopigwa au kujaribiwa na matokeo ya simu hizo;
2. Nakala za mawasiliano zilizotumwa kwako na majibu yoyote yaliyopokelewa; na
3. Kumbukumbu za kina za kutembelea nyumbani kwako au mahali pa kazi na matokeo ya utembeleaji huo.

Ikiwa wilaya ya shule itakosa kuandaa mkutano wa utatuzi ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea taarifa ya malalamiko yanayofuata mchakato **au** ikose kushiriki katika mkutano wa utatuzi, unaweza kumwomba ofisa anayesimamia kusikia suala lako aanze kuhesabu siku 45 za kalenda ya malalmiko yanayofuata mchakato.

**Nakala ya uamuzi unatumwa kwako na wilaya ya shule**

Ikiwa wewe na wilaya ya shule mmekubaliana kwa maandishi ili kutokuwa na mkutano wa usuluhishi, basi muda wa siku 45 za kalenda za mchakato wa kusikiliza malalamiko utaanza siku inayofuata.

Baada ya mwanzo wa usuluhishi au mkutano wa utatuzi na kabla ya mwisho wa kipindi cha utatuzi wa siku 30 za kalenda, ikiwa wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kwa kuandika kwamba hakuna makubaliano yanawezekana, basi muda wa siku 45 za kalenda ya usikilizaji unaofuata mchakato utaanza siku inayofuata.

Ikiwa wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kutumia mchakato wa usuluhishi lakini bado hamjaafikia makubaliano, mwishoni mwa kipindi cha utatuzi cha siku 30 za kalenda, mchakato wa usuluhishi unaweza kuendelea mpaka makubaliano yanapopatikana ikiwa pande zote mbili zitakubali kuendelea kwa kuandika. Hata hivyo, ikiwa wewe au wilaya ya shule itajiondoa kwenye mchakato wa usuluhishi wakati wa kipindi hiki, basi siku 45 za kalenda za mchakato wa kusikiliza malalamiko utaanza siku inayofuata

**Mkataba wa makubaliano ulioandikwa**

Ikiwa utatuzi wa mgogoro utapatikana katika mkutano wa utatuzi, wewe na wilaya ya shule lazima mfanye mkataba wa kisheria ambao:

1. Unatiwa saini na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule ambaye ana mamlaka ya kuiwakilisha wilaya ya shule; **na**
2. Unaweza kutekelezwa katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye mamlaka na uwezo (Mahakama ya Jimbo iliyo na mamlaka ya kusikiliza kesi kama hizo) au katika mahakama ya wilaya nchini Marekani au Idara ya Elimu Jimboni, ikiwa Jimbo lako lina utaratibu mwingine unaruhusu pande husika kutafuta utekelezaji wa mikataba ya utatuzi.

**Kipindi cha kukagua makubaliano**

Ikiwa wewe na wilaya ya shule mtakuwa na makubaliano ambayo ni matokeo ya mkutano wa utatuzi, kila upande (wewe au wilaya ya shule) unaweza kufutilia mbali makubaliano ndani ya siku tatu za kazi tangu wewe na wilaya ya shule mliposaini makubaliano.

# KUSIKILIZA MALALAMIKO YANAYOFUATA MCHAKATO

## UTARATIBU HURU WA KUSIKILIZA MALALAMIKO YANAYOFUATA MCHAKATO

**34 CFR §300.511 & K.A.R. 91-40-29(b)**

**Kwa Ujumla**

Wakati wowote malalamiko yanayofuata mchakato yanapowasilishwaa, wewe au wilaya ya shule inayohusika katika mgogoro lazima ipate fursa ya kusikilizwa katika mchakato huru jinsi inavyoelezwa katika sehemu za ***Malalamiko Yanayofuata Mchakato*** na ***Mchakato wa Utatuzi***.

**Ofisa wa kusikiliza asiyeegemea upande wowote**

Ofisa wa kusikiliza awe na sifa zisizopungua hizi:

1. Hafai kuwa mfanyakazi wa Idara ya Elimu Jimboni au wilaya ya shule ambayo inahusishwa katika elimu au huduma kwa mtoto husika. Hata hivyo, mtu si mfanyakazi wa idara hiyo ikiwa analipwa idara hiyo kuwa ofisa wa kusikiliza malalamiko;
2. Lazima asiwe na maslahi ya binafsi au ya kitaaluma ambayo yanaingiliana na malengo ya ofisa wa kusikiliza hoja.
3. Lazima awe na ufahamu na kuelewa masharti ya sheria ya IDEA, Kanuni za serikali za Taifa na Jimbo zinazohusiana na IDEA pamoja na fasili za kisheria za IDEA zilizotolewa na mahakama za Taifa na Jimbo; **na**
4. Lazima awe na ujuzi na uwezo wa kusikiliza, kufanya na kuandika maamuzi, kulingana na desturi wastani za kisheria.
5. ***** Ili kuhitimu kuwa ofisa wa kusikiliza malalamiko yanayofuata mchakato au kuwa ofisa wa mapitio ya serikali, mhusika lazima awe wakili aliye na kibali halali katika jimbo ambapo ana leseni ya kufaanya kazi ya taaluma ya sheria. K.A.R. 91-40-29(b)

Kila wilaya ya shule lazima iweka orodha ya watu ambao hufanya kazi ya maofisa wa kusikiliza usuluhishi, orodha hiyo lazima iwe na maelezo ya kuhitimu kwa ofisa husika.

**Hoja ya usikilizaji unaofuata mchakato**

Upande unaoomba kusikilizwa (wewe au wilaya ya shule) hauruhusiwi kuleta masuala ya kusikilizwa kwa kufuata mchakato ambao hayakujadiliwa katika malalamiko yanyofuata mchakato, isipokuwa upande mwingine husika ukubali.

**Muda wa kuomba kusikilizwa**

Wewe au wilaya ya shule lazima iombe kusikilizwa kwa namna isiyoegemea upande wowote wakati wa malalamiko yanayofuata mchakato ndani ya miaka miwili tangu wewe au wilaya ya shule ilipojua au ilipaswa kujua kuhusu suala linaloshughulikiwa katika malalamiko.

**Muda unaweza kurekebishwa kwa masharti**

Muda ulio hapa juu hatakubana ikiwa hukuweza kuwasilisha malalamiko yanayofuata mchakato ndani ya kipindi hicho kwa sababu:

1. Wilaya ya shule ilikosea kwa kudhani kwamba ilikuwa imetatua suala au tatizo unalotaja katika malalamiko; **au**
2. Wilaya ya shule haikukupa taarifa ilizofaa kukupatia kwa mujibu wa Sehemu ya B ya sheria ya IDEA.

## HAKI ZA KUSIKILIZWA

**34 CFR §300.512**

**Kwa Ujumla**

Una haki ya kujieleza mwenyewe katika kikao cha kusikilizwa kwa kufuata mchakato (ikiwa ni pamoja na kusikilizwa katika taratibu za kinidhamu) au katika kukata rufaa katika kusikilizwa ili kupokea ushahidi wa ziada, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa, ***Maamuzi ya rufaa; ukaguzi huria***. Aidha, upande wowote katika mchakato wa kusikilizwa una haki ya:

1. Kuandamana na kushauriwa na wakili au watu wenye ujuzi maalum au mafunzo kuhusu matatizo ya watoto wenye ulemavu;

2. Kuwakilishwa katika vikao na wakili;

3. Kuwasilisha ushahidi na kudadisi, kuhoji na kutaka mashahidi wahudhurie;

4. Kuzuia kuletwa kwa ushahidi wowote ambao ulikuwa haujafunuliwa kwa upande mwingine angalau siku tano za kazi kabla ya kusikilizwa;

5. Kupata maandishi, au, kwa chaguo lako, rekodi ya kielektroniki ya neno kwa neno ya kikao cha kusikilizwa; **na**

6. Kupata maandishi, au, kwa chaguo lako, nakala ya kielektriniki ya matokeo ya ufafanuzi na maamuzi.

**Ufichuzi wa ziada wa taarifa**

Zikiwa zimebaki angalau siku tano za kazi kabla ya kusikilizwa kwa kufuata mchakato, wewe na wilaya ya shule lazima mfichuliane tathmini zote zilizokamilishwa kufikia siku husika na mapendekezo kulingana na tathmini hizo ambazo wewe au wilaya ya shule una nia ya kutumia katika kusikilizwa.

Ofisa anayesimamia kusikilizwa au ofisa wa ukaguzi anaweza kuzuia upande wowote unaokosa kuzingatia masharti haya kuleta tathmini au mapendekezo husika wakati wa kusikilizwa bila idhini ya upande mwingine.

**Haki za mzazi katika kusikilizwa**

Lazima upewe haki ya:

1. Kuwa na mtoto wako wakati wa kusikilizwa;

2. Kuruhusu umma katika kikao cha kusikilizwa; **na**

3. Kupewa bila malipo rekodi ya kusikilizwa, matokeo ya ufafanuzi na maamuzi yaliyotolewa.

## MAAMUZI YA KUSIKILIZWA

**34 CFR §300.513**

**Uamuzi wa ofisa anayesikiliza**

Uamuzi wa ofisa anayesikiliza kuhusu ikiwa mtoto wako alipokea elimu ya umma inayofaa (FAPE) lazima itokane na ushahidi na hoja zinazohusiana na FAPE moja kwa moja.

Katika masuala yanayodai kuwepo kwa ukiukwaji wa kiutaratibu (kama vile "Timu ya IEP isiyo kamili"), ofisa anayesikiliza anaweza kufanya uamuzi kwamba mtoto wako hakupokea FAPE ikiwa tu ukiukaji wa kiutaratibu:

1. Uliingilia haki ya mtoto wako kupata elimu inayofaa ya umma bila malipo (FAPE);

2. Uliingilia kwa ukubwa fursa yako ya kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi unaohusiana na utoaji wa elimu inayofaa ya umma bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako; **au**

3. Umesababisha mtoto wako kunyimwa faida ya elimu.

Hakuna sharti lililotajwa hapo juu linaweza kufasiriwa ili kumzuia ofisa anayesikiliza kuagiza wilaya ya shule izingatie mahitaji yaliyo katika sehemu ya utaratibu wa ulinzi katika kanuni za Taifa chini ya Sehemu B ya sheria ya IDEA (34 CFR §§300.500 hadi 300.536).

Hakuna sharti chini ya vichwa: ***Kuwasilisha Malalamiko Yanayofuata Mchakato; Malalamiko Yanayofuata Mchakato; Fomu za Mfano; Mchakato wa Utatuzi; Utaratibu Huru wa Kusikiliza Malalamiko Yanayofuata Mchakato; Haki za Kusikilizwa; na Maamuzi ya Kusikilizwa*** (34 CFR §§300.507 hadi 300.513), yanaweza kuathiri haki yako ya kuwasilisha rufaa kwa Idara ya Elimu Jimboni dhidi ya uamuzi wa kusikilizwa kwa kufuata mchakato.

**Ombi tofauti la kusikilizwa kwa kufuata mchakato**

Hakuna sehemu katika utaratibu wa ulinzi ulio katika kanuni za Kitaifa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA (34 CFR §§300.500 hadi 300.536) inaweza kufasiliwa ili kukuzuia kuwasilisha malalamiko yanayofuata mchakato dhidi ya suala tofauti na malalamiko yanayofuata mchakato ambayo tayari yanaendelea.

**Matokeo na uamuzi unaotolewa kwa jopo la ushauri na umma**

Idara ya Elimu Jimboni au wilaya ya shule, (yoyote iliyohusika katika kusikilizwa kwako), baada ya kufuta taarifa yoyote inayoweza kutambulisha, lazima:

1. Itoe matokeo na maamuzi ya mchakato au ikate rufaa mbele ya jopo la ushauri wa elimu maalum Jimboni; **na**
2. Itoe matokeo na maamuzi hayo kwa umma.

# RUFAA

## UKAMILIFU WA UAMUZI; RUFAA; UKAGUZI HURIA

**34 CFR §300.514 & K.A.R. 91-40-51(f)**

**Ukamilifu wa mchakato wa kusikilizwa**

Uamuzi uliofanywa katika kusikilizwa kwa mchakato (ukiwa ni pamoja na kusikilizwa katika na taratibu za nidhamu) ni wa mwisho, ingawa kila upande uliohusika katika kusikilizwa (wewe au wilaya ya shule) unaweza kukata rufaa mbele ya Idara ya Elimu Jimboni.

*****Utaratibu wa malalamiko ya serikali unajumuisha haki ya mzazi au wilaya ya shule kukata rufaa dhidi ya matokeo au hitimisho za ripoti ya malalamiko. K.A.R. 91-40-51(f)

**Kukata rufaa; ukaguzi huria**

Ikiwa kuna upande (wewe au wilaya ya shule) ambao haukupendezwa (ulidhuriwa) na matokeo na uamuzi wa kusikilizwa, rufaa inaweza kuwasilishwa kwa Idara ya Elimu Jimboni.

Ikiwa kuna rufaa, Idara ya Elimu Jimboni lazima ifanye ukaguzi usioegemea upande wowote kwa matokeo na uamuzi uliokatiwa rufaa. Ofisa anayefanya ukaguzi lazima:

1. Achunguze rekodi nzima ya kusikilizwa;
2. Ahakikishe kwamba taratibu za kusikilizwa zilizingatia mahitaji ya mchakato;
3. Atafute ushahidi wa ziada ikiwa ni muhimu. Ikiwa kutakuwa na kikao cha kupokea ushahidi wa ziada, haki za kusikilizwa zilizoelezwa chini ya ***Haki za Kusikilizwa*** zinatumika;
4. Azipe pande husika fursa ya kujitetea kwa maneno au maandishi, au vyote, ikiwa ofisa wa ukaguzi atakubali;
5. Afanya uamuzi huria kuhusu kukamilika kwa ukaguzi; **na**
6. Akupe wewe na wilaya ya shule nakala ya maandiko, au, kwa chaguo lako, nakala ya kielektroniki ya matokeo ya maamuzi.

**Matokeo na uamuzi unaotolewa kwa jopo la ushauri na umma**

Idara ya Elimu Jimboni, baada ya kufuta taarifa zozote za binafsi zinazoweza kutambulisha, lazima:

1. Iwasilishe matokeo na maamuzi ya rufaa kwa jopo la ushauri wa elimu maalum katika Jimbo; **na**
2. Itoe matokeo na maamuzi hayo kwa umma.

**Ukamilifu wa maamuzi ya ukaguzi**

Uamuzi uliofanywa na ofisa wa uhakiki ni wa mwisho isipokuwa wewe au wilaya ya shule ichague kufuata mkondo wa mahakama, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa ***Mashtaka ya Kiraia, Ikiwemo Kipindi cha Muda wa Kuanzisha Mashtaka Hayo***.

## MUDA NA URAHISI WA KUSIKILIZWA NA UKAGUZI

**34 CFR §300.515**

Wilaya ya shule lazima ihakikisha kwamba kabla ya kuisha kwa siku 45 za kalenda baada ya kumalizika kwa kipindi cha siku 30 za kalenda za kufanya mkutano wa maamuzi **au**, kama ilivyoelezwa chini ya mada ndogo ya ***Nakala ya uamuzi unatumwa kwako na wilaya ya shule,*** bila kupita siku 45 za kalenda baada ya kumalizika kwa kipindi cha kurekebisha muda:

1. Uamuzi wa mwisho unafanyika katika kusikilizwa; **na**
2. Nakala ya uamuzi unatumwa kwa barua pepe kwako na wilaya ya shule.

Idara ya Elimu Jimboni lazima ihakikisha kwamba ndani ya siku 30 za kalenda baada ya kupokea ombi la ukaguzi:

1. Uamuzi wa mwisho unafanyika katika ukaguzi; **na**
2. Nakala ya uamuzi unatumwa kwako na wilaya ya shule.

Ofisa wa kusikiliza au wa ukaguzi anaweza akaongeza muda maalum wa zaidi juu ya vipindi vilivyotajwa hapo juu (siku 45 za kalenda kwa ajili ya kusikiliza ili kupata uamuzi na siku 30 za kalenda kwa ukaguzi wa uamuzi) ikiwa wewe au wilaya ya shule itaomba kuongezewa muda.

Kila kkikao cha ukaguzi kinachohusisha hoja zinazowasilishwa kwa maneno lazima ufanyike kwa wakati na mahali ambayo ni rahisi kwako na mtoto wako.

## MASHTAKA YA KIRAIA, IKIWEMO KIPINDI CHA MUDA WA KUANZISHA MASHTAKA HAYO

**34 CFR §300.516**

**Kwa Ujumla**

Upande wowote (wewe au wilaya ya shule) ambao hakubaliani na matokeo na uamuzi katika ukaguzi katika ngazi ya Jimbo una haki ya kuanzisha shtaka la kirai linalohusiana na jambo ambalo lilikuwa hoja ya kusikilizwa kwa kufuata mchakato (ikiwa ni pamoja na kusikiliza hoja zinazohusiana na taratibu za nidhamu). Shtaka linaweza kuwasilishwa katika mahakama ya Jimbo yenye mamlaka na uwezo (mahakamani ambayo ina mamlaka chini ya sheria ya Majimbo kusikiliza aina hizo za kesi) au katika mahakama ya wilaya nchini Marekani.

**Vikwazo vya muda**

> *Upande huskika (wewe au wilaya ya shule) unaochukua hatua hiyo utakuwa na siku 30 za kalenda tangu tarehe ya uamuzi wa ofisa wa ukaguzi Jimboni ili kuwasilisha shtaka la kiraia (KSA 72-974 (d)).

**Taratibu za ziada**

Katika kesi yoyote ya kiraia, mahakama:

1. Hupokea kumbukumbu za michakato ya kiusimamizi;
2. Husikiliza ushahidi wa ziada kwa ombi lako au ombi la wilaya ya shule; **<u>na</u>**
3. Hufanya maamuzi yake kwa kuzingatia uzito wa ushahidi na kukata shauri ambalo mahakama inaona kuwa sahihi.

Katika hali zinazoruhusu, uamuzi wa mahakama unaweza kujumuisha kurudishiwa malipo ya shule ya binafsi na huduma za fidia za kielimu.

**Mamlaka ya mahakama za wilaya**

Mahakama ya wilaya nchini Marekani ina mamlaka ya kufanya uamuzi juu ya hatua zilizoletwa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA bila kujali kiasi cha mgogoro.

**Sheria ya ufafanuzi**

Hakuna kipengele katika Sehemu ya B ya sheria ya IDEA inakataza au kuzuia haki, taratibu na usuluhishi unaopatikana chini ya Katiba ya Marekani, Sheria ya Marekani na Ulemavu ya mwaka 1990, Kifungu cha V cha Sheria ya Kurekebisha Tabia cha 1973 (Sehemu ya 504), au sheria nyingine za Taifa kulinda haki kwa watoto wenye ulemavu, isipokuwa kuwa kwamba, kabla ya kuwasilisha shtaka la kiraia chini ya sheria hizi ili kutafuta haki inayopatikana pia katika Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, michakato zilizoelezwa hapo juu lazima ifanywe kwa kiwango sawa na vile ambavyo upande husika ungetenda chini ya Sehemu B ya sheria ya IDEA. Hii ina maana kwamba unaweza kuwa nahaki zinazopatikana chini ya sheria nyingine ambazo zinaingiliana na zinazopatikana chini ya sheria ya IDEA, lakini kwa ujumla, ili kupata haki chini ya sheria hizo, lazima kwanza utumie usuluhishi wa utawala uliopo chini ya IDEA (yana ni, malalamiko yanayofuata mchakato; mchakato wa utatuzi, ikiwa ni pamoja na mkutano wa utatuzi, na taratibu za kusikia zisizofaa kwa utaratibu) kabla ya kwenda moja kwa moja kwenye mahakamani.

## KITUO CHA MTOTO WAKATI WA KUSUBRI UTARATIBU WA MALALAMIKO NA KUSIKILIZWA KWA KUFUATA MCHAKATO

**34 CFR §300.518**

Isipokuwa kama ilivyoandikwa chini ya kichwa ***UTARATIBU WA KUWAADHIBU WATOTO WENYE ULEMAVU,*** mara baada ya malalamiko yanayofuata mchakato kutumwa kwa upande mwingine husika, wakati wa mchakato wa utatuzi, na wakati wa kusubiri uamuzi wa mchakato usikilizaji usioegemea upande wowote au uamuzi wa mahakama, isipokuwa wewe na Jimbo au wilaya ya shule mkubaliane vinginevyo, mtoto wako lazima abaki katika kituo chake cha sasa cha elimu.

Ikiwa malalamiko yanayofuata mchakato yanahusisha ombi la awali kuwa katika shule ya umma, mtoto wako, kwa idhini yako, lazima asajiliwe katika mpango wa kawaida wa shule ya umma mpaka kukamilika kwa michakato yote ya kusikilizwa.

Ikiwa malalamiko yanayofuata mchakato yanahusu ombi la huduma za awali chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA kwa mtoto anayebadilishwa kutoka kuhudumiwa chini ya Sehemu ya C ya IDEA kwenda Sehemu B ya IDEA na ambaye hawezi tena kuwa katika huduma za Sehemu ya C kwa sababu mtoto ametimiza miaka mitatu, wilaya ya shule haipaswi kutoa huduma za Sehemu ya C ambazo mtoto amekuwa akipokea. Ikiwa mtoto anaonekana kwamba anastahiki chini ya Sehemu B ya IDEA na unakubali mtoto wako apate elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, basi, wakati wa kusubiri matokeo ya mchakato, wilaya ya shule lazima impe elimu maalum na huduma zinazohusiana ambazo hazipingwi (yale ambayo wewe na wilaya ya shule mnakubaliana kuyahusu).

Ikiwa ofisa wa ukaguzi wa Jimbo katika mchakato wa rufaa ya usimamizi atakubaliana na wewe kwamba mabadiliko ya mahali mtoto anaposoma yanafaa, mabadiliko hayo lazima yafanyike mahali mtoto wako anaposoma sasa ambapo atabaki huku akisubiri uamuzi wa wa mchakato wa kusikilizwa unaoendelea au hatua ya mahakama.

## ADA ZA WAKILI

**34 CFR §300.517**

**Kwa Ujumla**

Katika hatua yoyote au shauri linaloletwa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, mahakama, kwa hiari yake, inaweza ikakutoza ada inayofaa za wanasheria kama sehemu ya gharama kwako, ikiwa ume (kushinda).

Katika hatua yoyote au mchakato unaoanzishwa chini ya Sehemu ya B ya sheria ya IDEA, mahakama, kwa hiari yake, inaweza kuweka ada ya wakili inayoona ni nzuri kama sehemu ya gharama kwa Idara ya Elimu Jimboni au wilaya ya shule, ili kulipwa na wakili wako, ikiwa wakili: (a) atawasilsiha malalamiko au kesi ambayo mahakama itaona kuwa mzaha, isiyofaa, au isiyo na msingi; **au** (b) anaendelea kujadili suala baada ya madai hayo kutajwa kuwa, yasiyo ya maana, au yasiyo na msingi; **au**

Katika hatua yoyote au shauri linaloletwa chini ya Sehemu B ya sheria ya IDEA, mahakama, kwa hiari yake, inaweza kuweka ada za wanasheria kama sehemu ya gharama kwa Idara ya Elimu Jimboni au wilaya ya shule, ili uilipe wewe au wakili wako, ikiwa ombi lako la usikilizaji unaofuata mchakato au kesi ya baadaye ya kisheria iliwasilishwa kwa madhumuni yasiyofaa, kama vile kusumbua, kusababisha ucheleweshaji usiohitajika, au kwa kiasi kikubwa kuongeza gharama ya hatua au shauri (kusikilizwa).

**Kuagizwa kulipa ada**

Mahakama inaweza kuagiza kiasi cha ada stahiki kwa wakili kama ifuatavyo:

1. Malipo lazima yawe kulingana na viwango vilivyomo katika jamii ambapo shauri au utaratibu ulianzishwa na kwa aina na ubora wa huduma zilizotolewa. Hakuna bonasi au kizidisho kinaweza kutumika kuhesabu ada iliyotolewa.

2. Ada za mwanasheria haziwezi kutolewa na gharama zinazohusiana haziwezi kulipwa katika shauri lolote au mchakato ulio chini ya Sehemu ya B ya IDEA kwa huduma zilizofanyika baada ya suluhu ya maandishi kuwasilishwa kwako ikiwa:

    a. Suluhu ilitolewa ndani ya wakati uliowekwa na Kanuni ya 68 ya Kanuni za Taifa za Utaratibu wa Kesi za kiraia au, katika hali ya kusikilizwa kwa kufuata mchakato au ukaguzi wa ngazi ya Jimbo, wakati wowote zaidi ya siku 10 za kalenda kabla ya kuanza;

    b. Suluhu halijakubalika ndani ya siku 10 za kalenda; **na**

    c. Ofisa wa mahakama au ofisa wa utawala anaona kwamba suluhu ulilopata si bora kwako zaidi kuliko pendekezo la utatuzi.

    Licha ya vikwazo hivi, ada kwa wanasheria na gharama zinazohusiana zinaweza kufanywa kwako ikiwa umeshinda kesi na ulikuwa na haki ya kukataa pendekezo la utatuzi.

3. Malipo hayawezi kutolewa kuhusiana na mkutano wowote wa Timu ya Mpango Mahususi kwa Elimu ya Mtoto (IEP) isipokuwa mkutano huo unafanyika kama matokeo ya utaratibu wa utawala au hatua ya mahakama.

4. Ada pia hazitaagizwa kwa usuluhishi kama ilivyoelezwa chini ya sehemu ya Usuluhishi.

Mkutano wa usuluhishi, kama ilivyoelezwa chini ya ***Mchakato wa Utatuzi***, hauchukuliwi kuwa mkutano ulioandaliwa kama matokeo ya kusikilizwa kwa utawala au hatua za mahakamani, na pia hauchukuliwi kuwa kusikilizwa kwa utawala au hatua ya mahakama kwa madhumuni ya ada za wakili.

Mahakama hupunguza, kama inavyofaa, kiasi cha ada za wakili zilizotolewa chini ya Sehemu B ya sheria ya IDEA, ikiwa mahakama itaona kwamba:

1. Wewe, au wakili wako, wakati wa hatua au usikilizaji, ucheleweshaji kwa namna isiyofaa utatuzi wa mwisho wa mgogoro;

2. Kiasi cha ada za wakili kilichoidhinishwa ni zaidi ya kiwango cha malipo kwa saa moja kinachokubalika katika jamii kwa huduma sawa miongoni mwa wanasheria wa ujuzi sawa, sifa na uzoefu;

3. Wakati uliotumika na huduma za kisheria zilizotolewa zilikuwa nyingi kwa kuzingatia hali ya shauri au mchakato; **<u>au</u>**

4. Mwanasheria anayewakilisha hakuipa wilaya ya shule taarifa muhimu kwa mchakato wa usuluhishi, kama ilivyoelezwa chini ya kichwa cha ***Malalamiko Yanayofuata Mchakato*** .

Hata hivyo, mahakama huenda haitapunguza ada ikiwa mahakama itapata kuwa Jimbo au wilaya ya shule imesitisha uamuzi wa mwisho wa hatua au kusikilizwa au kulikuwa na ukiukwaji chini ya masharti ya utaratibu wa ulinzi katika Sehemu B ya IDEA.

# UTARATIBU WA KUWAADHIBU WATOTO WENYE ULEMAVU

## MAMLAKA YA WAFANYAKAZI WA SHULE

**34 CFR §300.530**

**Uamuzi wa kila tukio kivyake**

Wafanyakazi wa shule wanaweza kuzingatia hali yoyote ya kipekee kwa msingi wa tukio kwa tukio wakati wa kuamua kama mabadiliko ya mahali anaposoma mototo yaliyotolewa kulingana na mahitaji yafuatayo yanayohusiana na nidhamu ni sahihi kwa mtoto mwenye ulemavu ambaye amevunja kanuni za shule kwa wanafunzi.

**Kwa Ujumla**

Kwa kuwa wanaweza kuwachukulia hatua kama hiyo watoto wasio na ulemavu, wafanyakazi wa shule wanaweza, kwa muda usiozidi **siku 10 za shule**, kumwaondoe mtoto mwenye ulemavu ambaye anakiuka kanuni ya mwongozo wa wanafunzi kutoka mahali anapohudumiwa kwa sasa hadi katika mpangilio sahihi wa mpito, mpangilio mwingine, au kumsimamisha. Wafanyakazi wa shule pia wanaweza kumwondoa tena mtoto kwa **siku zisizo zidi 10 za shule** mfululizo katika mwaka huo huo wa shule kwa ajili ya matukio tofauti ya utovu, mradi kuondolewa huko hakusababishi mabadiliko ya mahali mtoto anaposoma (tazama kichwa cha ***Mabadiliko ya Mahali pa Kusoma kwa Sababu za Nidhamu*** kwa ufafanuzi).

Matoto aliye na ulemavu akishaondolewa mahali anaposomea kwa sasa kwa jumla ya **siku 10 za shule** katika mwaka huo huo wa shule, wilaya ya shule lazima, ifanye hivi katika tukio jingine la kuondolewa katika mwaka ule ule wa shule, itoa huduma kwa kiwango kinachohitajika ilivyotajwa hapa chini cha ***Huduma***.

**Mamlaka ya ziada**

Ikiwa tabia iliyovunja kanuni za wanafunzi si dalili ya ulemavu wa mtoto (angalia kichwa kidogo ***kutambua Kujitokeza***) na mabadiliko kwa ajili ya adhabu yangezidi **siku 10 za shule** mfululizo, wafanyakazi wa shule wanaweza kutumia taratibu za nidhamu kwa mtoto aliye na ulemavu kwa namna ile ile na kwa kipindi sawa na cha watoto wasiokuwa na ulemavu, ingawa shule inapaswa kutoa huduma kwa mtoto huyo kama ilivyoelezwa hapa chini ya ***Huduma***. Timu ya Mpango Mahususi kwa Elimu ya Mtoto (IEP) huamua mpangilio mbadala wa mpito wa huduma kama hizo.

**Huduma**

Wilaya ya shule haipaswi kutoa huduma kwa mtoto mwenye ulemavu au mtoto asiye na ulemavu ambaye ameondolewa kwenye sehemu yake ya sasa ya elimu kwa **siku 10 za shule au chini** ndani ya mwaka ule ule wa shule.

Mtoto mwenye ulemavu ambaye ameondolewa katika mahali pake pa sasa kwa **zaidi ya siku 10** na tabia haihusiani na ulemavu wake (angalia kichwa kidogo, ***Kutambua kujitokeza*** ) au ambaye ameondolewa chini ya hali maalum (angalia sehemu ndogo, ***Hali maalum***) lazima:

1. Aendelee kupokea huduma za elimu (awe na chaguo la elimu ya bure ya umma inayofaa), ili kumwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, ingawa katika mazingira mengine (ambayo inaweza kuwa mpangilio wa mpangilio wa elimu wa muda mfupi), na kuendelea kuelekea kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto; <u>**na**</u>

2. Apate, kama inavyofaa, tathmini ya tabia, na huduma za kusawazisha na kuboresha tabia, ambayo yamepangwa kushughulikia ukiukaji wa tabia ili yasitokee tena.

Baada ya mtoto aliye na ulemavu kuondolewa sehemu yake ya sasa kwa **siku 10 za shule** katika mwaka huo huo wa shule, na <u>**ikiwa**</u> kuondolewa kwa sasa ni kwa **siku 10 za shule** kwa safu au chini **na** ikiwa kuondolewa si mabadiliko ya mahali anaposoma (tazama ufafanuzi hapa chini), <u>**basi**</u> viongozi wa shule, ikiwa ni pamoja na msimamizi wa elimu ya kawaida; mkurugenzi wa elimu maalum au wafanyakazi walioteuliwa na mkurugenzi; na mwalimu wa watoto wanaohitaji elimu maalum (KAR 91-40-33 (b)), wabainishe kiwango ambacho huduma zinahitajika ili mtoto aendelee kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, ingawa katika mazingira mengine na aendelee kuelekea kutimiza malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto.

Ikiwa kuondolewa ni mabadiliko ya mahali ambapo mtoto anasoma (angalia kichwa, ***Mabadiliko ya Mahali pa Kusoma kwa Sababu za Nidhamu*** ), Timu ya IEP ya mtoto huamua huduma zinazofaa ili kumwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa elimu ya jumla, ingawa katika mazingira mengine (ambayo yanaweza kuwa mpangilio wa elimu mbadala kwa muda mfupi), na aendelee kuelekea kutimiza malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto.

**Utambuzi wa kujitokeza**

Ndani ya **siku 10 za shule** baada ya uamuzi wowote wa kubadili mazingira ya masomo kwa mtoto mwenye ulemavu kwa sababu amekiuka kanuni za mwenendo wa wanafunzi (isipokuwa katika hali ya kuondolewa kwa **siku 10 za shule** zinazofuatana au zisizofika siku hizo hazihusishi mabadiliko ya mazingira) , wilaya ya shule, wewe, na wanajopo wengine husika wa Timu ya IEP (kama ilivyoainishwa na wewe na wilaya ya shule) lazima mkague taarifa zote zinazofaa katika faili la mwanafunzi, ikiwa ni pamoja na IEP ya mtoto, uchunguzi wowote uliofanywa na mwalimu, na taarifa yoyote inayofaa inayotolewa na wewe ili kuamua:

1. Ikiwa mwenendo husika unasababishwa na, au ulikuwa na uhusiano mkubwa wa moja kwa moja na ulemavu wa mtoto; **<u>au</u>**

2. Ikiwa mwenendo husika ulikuwa matokeo ya moja kwa moja ya kushindwa kwa wilaya ya shule kutekeleza mpango mahususi kwa elimu ya mtoto (IEP).

Ikiwa wilaya ya shule, wewe, na mwanajopo mwingine husika wa Timu ya IEP ya mtoto mtaamua kwamba mojawapo ya masharti hayo yametimizwa, tabia hiyo inapaswa kuchukuliwa kuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto.

Ikiwa wilaya ya shule, wewe, na wanajopo wengine husika wa Timu ya IEP ya mtoto mtaamua kwamba tabia husika ni matokeo ya moja kwa moja ya kushindwa kwa wilaya ya shule kutekeleza mpango mahususi kwa elimu ya mtoto (IEP), wilaya ya shule lazima ichukue hatua ya haraka ili kukabiliana na upungufu huo.

**Uamuzi kwamba tabia ni dhihirisho la ulemavu wa mtoto**

Ikiwa wilaya ya shule, wewe, na wanajopo wengine husika wa Timu ya IEP mtaamua kwamba tabia husika ni dhihirisho la ulemavu wa mtoto, Timu ya IEP lazima:

1. Ifanye tathmini ya utendaji, isipokuwa kama wilaya ya shule ilikuwa imefanya tathmini ya tabia kabla ya tabia ambayo imesababisha mabadiliko ya mazingira, na kutekeleza mpango wa kurekebisha tabia ya mtoto; **<u>au</u>**

2. Ikiwa mpango wa kurekebisha tabia tayari unatekelezwa, tathmini mpya ya mpango huo wa urekebishaji, ikiwa inafaa, ufanyike ili kushughulikia tabia.

Isipokuwa kama ilivyoelezwa hapa chini kwenye mada ndogo ya Mazingira ***maalum***, wilaya ya shule lazima imrudishe mtoto wako katika mazingira ambayo mtoto wako ameondolewa, isipokuwa wewe na wilaya mkubali kwamba mabadiliko ya mazingira ni sehemu ya mabadiliko ya mpango wa kurekebisha tabia.

**Hali maalum**

Ikiwa tabia hiyo ilikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto wako au la, wafanyakazi wa shule wanaweza kumwondoa mwanafunzi katika mpango jumuishi wa elimu mbadala (uliowekwa na Timu ya IEP ya mtoto) kwa muda usiozidi siku 45 za shule, ikiwa mtoto wako:

1. Alileta silaha (angalia ufafanuzi hapa chini) shuleni au ana silaha shuleni, katika majengo ya shule, au katika tukio la shule lililo chini ya mamlaka ya Idara ya Elimu Jimboni au wilaya ya shule;

2. Kwa kujua anayo au anatumia dawa za kulevya (tazama ufafanuzi hapa chini), au anauza au anafanikisha uuzaji wa dutu zinazodhibitiwa, (angalia ufafanuzi hapa chini), wakati wa shule, kwenye majengo ya shule, au katika tukio la shule chini ya mamlaka ya Idara ya Elimu Jimboni au wilaya ya shule; **<u>au</u>**

3. Amesababisha maumivu makubwa ya mwili (angalia ufafanuzi hapa chini) kwa mtu mwingine wakati wa shuleni, katika majengo ya shule, au katika tukio la shule lililo chini ya mamlaka ya Idara ya Elimu Jimboni au wilaya ya shule.

**Fasili**

*Dutu zinazodhibitiwa* inamaanisha dawa za kulevya au dutu nyingine inavyotambuliwa chini ya ratiba I, II, III, IV, au V katika kifungu cha 202 (c) cha Sheria ya Dutu Zinazodhibitiwa (21 USC 812 c)).

*Dawa zilizopogwa marufuku* ina maanisha dutu zinazodhibitiwa; lakini haijumuishi dutu zinazodhibitiwa ambazo zinamiliki kisheria au zinatumiwa chini ya usimamizi wa mtaalamu wa afya aliye na leseni au ambayo inamilikiwa kisheria au kutumika chini ya mamlaka yoyote chini ya Sheria hiyo au chini ya sheria nyingine yoyote ya Sheria za Taifa.

*Maumivu makubwa ya mwili* ina maana iliyotolewa kwenye "maumivu makubwa ya mwili " chini ya aya ya (3) ya kifungu kidogo (h) cha kifungu cha 1365 cha kichwa cha 18, Kanuni za Marekani.

*Silaha* ina maana iliyopewa neno "silaha hatari" chini ya aya (2) ya kifungu cha kwanza kidogo (g) cha kifungu cha 930 cha kichwa cha 18, Kanuni za Marekani.

**Kuarifiwa**

Katika siku ya kufanya uamuzi wa kuondoa mabadiliko ya mazingira ya mtoto wako kwa sababu ya ukiukwaji wa kanuni ya mwenendo wa wanafunzi, wilaya ya shule lazima ikujulishe kuhusu uamuzi huo, na kukupa taarifa ya utaratibu wa ulinzi.

## MABADILIKO YA MAHALI PA KUSOMA KWA SABABU ZA NIDHAMU

**34 CFR §300.536**

Uondoaji wa mtoto wako mwenye ulemavu kutoka mazingira yake ya sasa ya elimu ni **badiliko la mahali pa kusoma** ikiwa:

1. Uondoaji hhuo ni zaidi ya siku 10 za shule mfululizo; **au**
2. Mtoto wako amekuwa akifanyiwa mfululizo wa mabadiliko ambayo yanafuata ruwaza kwa sababu:
    a. Mfululizo wa jumla ya kuondolewa unafiukia siku 10 za shule katika mwaka wa shule;
    b. Tabia ya mtoto wako ni sawa na tabia aliyokuwa nayo katika matukio ya awali yaliyotokana na mfululizo wa kuondolewa; na
    c. Kuna masuala ya ziada kama urefu wa kila kuondolewa, kiasi cha muda ambao mtoto wako ameondolewa na ukaribu wa uondoaji kwa kila uondoaji mwingine.

Uamuzi ikiwa mfululizo wa uondoaji unachukuliwa kuwa mabadiliko ya mazingira hutegemea kila tukio kivyake kulingana na maoni ya wilaya ya shule na, ikiwa itapingwa, inaweza kukaguliwa kupitia mchakato stahiki na kesi za mahakama.

## UAMUZI WA MAZINGIRA

**34 CFR § 300.531**

Timu ya mpango mahususi kwa elimu ya mtoto (IEP) huamua mpangilio wa elimu mbadala ambao ni **mabadiliko ya mahali pa mtoto kusomea** , na mabadiliko mengine kwa mujibu kichwa kidogo ***Mamlaka ya ziada*** na ***hali Maalum*** .

## RUFAA

**34 CFR § 300.532**

**Kwa Ujumla**

Unaweza kuwasilisha malalamiko yanayofuata mchakato (tazama ***Utaratibu wa Malalamiko Yanayofuata Mchakato*** ) ili uombe kusikilizwa kwa kufuata mchakato ikiwa hukubaliani na:

1. Uamuzi wowote kuhusu mahali pa mtoto wako kusomea unaofanywa chini ya masharti haya ya nidhamu; **au**
2. Uamuzi kwamba tabia ni dhihirisho la ulemavu

Wilaya ya shule inaweza kufungua malalamiko yanayofuata mchakato (angalia hapo juu) ili kuomba kusikilizwa kwa kufuata mchakato ikiwa inaamini kuwa mazingira ya sasa ya mtoto wako yana uwezekano mkubwa wa kusababisha madhara kwa mtoto wako au kwa wengine.

**Mamlaka ya ofisa anayesikiliza**

Ofisa wa kusikiliza aliye na sifa zilizotajwa katika kichwa kidogo ***Ofisa wa kusikilkiza asiyeegemea upande wowote*** sharti aongoze vikao vya kusikiliza na afanye uamuzi. Ofisa wa kusikiliza anaweza:

1. Akamrudisha mtoto wako mwenye ulemavu kwenye mpango wa elimu ambao mtoto wako aliondolewa ikiwa ofisa wa kusikiliza anmeona kuwa kuondolewa kulikuwa ukiukaji wa mahitaji yaliyoelezwa chini ya ***Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule*** , au kwamba tabia ya mtoto wako ilikuwa dhihirisho la ulemavu wa mtoto wako ; **au**

2. Akaamrisha mabadiliko ya mahali pa mtoto wako mwenye ulemavu kusoma kwenye mazingira sahihi ya mpangilio wa muda mfupi kwa muda usiozaidi siku 45 za shule ikiwa ofisa wa kusikiliza anaona kuwa mazingira ya sasa ya mtoto wako yana uwezekano mkubwa wa kusababisha madhara kwa mtoto wako au kwa wengine..

Taratibu hizi za kusikilia zinaweza kurudia, ikiwa wilaya ya shule inaamini kwamba kurudi kwa mtoto wako katika mazingira ya awali kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha madhara kwa mtoto wako au kwa wengine.

Wakati wowote wewe au wilaya ya shule inapowasilisha malalamiko yanayofuata mchakato ili kuomba kusikia suala kama hilo, kikao cha kusikilizwa ambacho kinakidhi mahitaji yaliyoelezwa chini ya kichwa cha ***Utaratibu wa Malalamiko Yanayofuata Mchakato, Kusikiliza Malalamiko Yanayofuata Mchakato na Utaratibu*** wa ***Rufaa ya maamuzi; ukaguzi usiopendelea upande wowote,*** isipokuwa katika hali ifuatavyo:

1. Idara ya Elimu Jimboni au wilaya ya shule sharti ipangie mchakato wa kusikilizwa, ambacho sharti kiwe ndani ya **siku 20** za shule baada ya kikao cha kusikilizwa kuombwa na lazima iamuliwe ndani ya siku **10** za shule baada ya kikao.

2. Isipokuwa kama wewe na wilaya ya shule mmekubaliana kwa maandishi ili kutokuwa na mkutano wa utatuzi, mkutano wa usuluhishi sharti ufanyike ndani ya siku **saba** za kalenda baada ya kupokea ilani ya malalamiko yanayofuata mchakato. Mchakato wa kusikiliza unaweza kuendelea isipokuwa kama suala limetatuliwa na kuridhiwa na pande zote mbili ndani ya siku **15** kalenda baada ya kupokea malalamiko yanayofuata mchakato.

3. Jimbo linaweza kuanzisha sheria tofauti za utaratibu wa kusikilizwa kwa mchakato ambazo ni tofauti na zilizopo kwa ajili ya michakato mingine ya kusikilizwa, sheria hizo lazima ziwe zifuatazo na sheria zilizo katika waraka huu kuhusu kusikilizwa kwa kufuata mchakato, isipokuwa kwa muda.

Wewe au wilaya ya shule inaweza kukata rufaa kwa uamuzi wa mchakato ulioharakishwa kwa njia sawa na ilivyo katika michakato mingine ya kusikilizwa (angalia ***kukata Rufaa***).

## MAHALI PA KUSOMEA WAKATI WA RUFAA

**34 CFR §300.533**

Ikitokea, kama ilivyoelezwa hapo juu, wewe au wilaya ya shule iwasilishe malalamiko yanayofuata mchakato kuhusiana na mambo ya kimaadili, mtoto wako lazima (isipokuwa wewe na Idara ya Elimu Jimboni au wilaya ya shule mkubaliane vinginevyo) abaki katika mipangilio wa elimu wa muda mfupi akisubiri uamuzi wa ofisa wa kusikiliza, au mpaka mwisho wa kipindi cha kuondolewa kama ilivyoelezwa na kuelezewa chini ya ***Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule*** , kutegemea kinachotokea kwanza.

## ULINZI KWA WATOTO WASIOSTAHIKI ELIMU MAALUM NA HUDUMA ZINAZOHUSIANA

**34 CFR §300.534**

**Kwa Ujumla**

Ikiwa mtoto wako amebainishwa kwamba anastahiki elimu maalum na huduma zinazohusiana na akiuke kanuni ya mwenendo wa wanafunzi, lakini wilaya ya shule ifahamu (kama ilivyoelezwa hapo chini) kabla ya tabia iliyosababisha uvunjifu wa mwongozo kutokea, kwamba mtoto wako alikuwa mwenye ulemavu, basi mtoto wako anaweza akatumia haki zozote za ulinzi ilivyoelezwa katika taarifa hii.

**Msingi wa ufahamu kwa masuala ya nidhamu**

Wilaya ya shule itachukuliwa kuwa na ufahamu kwamba mtoto wako ni mwenye ulemavu ikiwa, kabla ya tabia iliyosababisha hatua ya nidhamu kuchukuliwa:

1. Uliwasilsiha dukuduku lako kwa maandishi kwa wafanyakazi wa usimamizi au wa utawala wa idara ya elimu, au kwa mwalimu wa mtoto wako kwamba mtoto wako anahitaji elimu maalum na huduma zinazohusiana;

2. Umeomba tathmini inayohusiana na ustahiki wa kupata elimu maalum na huduma zinazohusiana; **au**

3. Mwalimu wa mtoto wako au wafanyakazi wengine wa wilaya ya shule walielezea dukuduku mahususi kuhusu tabia iliyoonyeshwa na mtoto wako kwa mkurugenzi wa wilaya ya shule anayehusika na elimu maalum au kwa wafanyakazi wengine wa wilaya ya shule.

**Upekee**

Wilaya ya shule haitachukuliwa kuwa ilifahamu hali hizo iwapo:

1. Hujaruhusu tathmini ya mtoto wako au umekataa huduma za elimu maalum; **au**

2. Mtoto wako ametathminiwa na ikaamuliwa kuwa ni mtoto mwenye ulemavu chini ya Sehemu B ya sheria ya IDEA.

**Masharti yanayotumika ikiwa hakuna msingi wa ufahamu**

Ikiwa kabla ya kuchukua hatua za nidhamu dhidi ya mtoto wako, wilaya ya shule haijui kwamba mtoto wako ni mwenye ulemavu, kama ilivyoelezwa chini ya vichwa ***Msingi wa ufahamu kwa masuala ya nidhamu*** na ***Upekee*** , mtoto wako anaweza kuchukuliwa hatua za nidhamu zinazotumiwa kwa watoto wasio na ulemavu wanaohusika katika tabia kama alizotenda.

Hata hivyo, ikiwa ombi la tathmini ya mtoto wako limefanywa wakati mtoto wako anachukuliwa hatua za nidhamu, tathmini lazima ifanyike kwa namna inayoharakishwa.

Hadi tathmini itakapokamilika, mtoto wako ataendelea kuwa katika mazingira ya elimu aliyowekwa na mamlaka ya shule, ambayo inaweza kuhusisha kusimamishwa au kufukuzwa bila huduma za elimu.

Ikiamuliwa kuwa mtoto wako ni mwenye ulemavu, ikizingatiwa habari kutoka kwa tathmini iliyofanywa na wilaya ya shule, na taarifa iliyotolewa na wewe, wilaya ya shule lazima itoe elimu maalum na huduma zinazohusiana kulingana na Sehemu B ya sheria ya IDEA, ikiwa ni pamoja na mahitaji ya nidhamu ilivyoelezwa hapo juu.

## Kuelekezwa pamoja na Hatua Zinazochukuliwa na Maofisa wa Utekelezaji wa Sheria na Mahakama

**34 CFR §300.535**

Sehemu B ya sheria ya IDEA haikatazi:

1. Shirika kutoa taarifa ya uhalifu uliofanywa na mtoto mwenye ulemavu kwa mamlaka husika; **au**

2. Utekelezaji wa sheria na mamlaka ya mahakama kutokana na kutekeleza majukumu yao kuhusiana na utekelezaji wa sheria ya Serikali ya Jimbo na Taifa kwa uhalifu uliofanywa na mtoto mwenye ulemavu.

**Kuwasilisha rekodi**

Ikiwa wilaya ya shule itaripoti uhalifu uliofanywa na mtoto mwenye ulemavu, wilaya ya shule:

1. Lazima ihakikishe kwamba nakala za rekodi ya elimu maalum ya mtoto na za nidhamu zinawasilishwa ili zizingatiwe na mamlaka ambapo uhalifu unaripotiwa; **na**

2. Inaweza kupeleka nakala za rekodi ya elimu maalum ya mtoto na rekodi za hatua za nidhamu kwa kiasi ambacho kinaruhusiwa na Sheria ya Haki na Faragha ya Familia katika Elimu (FERPA).

# MASHARTI YA KUCHUKUA UAMUZI WA MOJA KWA MOJA UNAOCHUKULIWA NA WAZAZI WA WATOTO WALIO KATIKA SHULE ZA BINAFSI KWA GHARAMA ZA UMMA

## MASHARTI YA SERIKALI YA TAIFA KWA WATOTO WALIOSAJILIWA KATIKA SHULE ZA BINAFSI KWA HIARI

**34 CFR §300.131 through 34 CFR §144**

Sehemu ya B ya sheria ya IDEA haihitaji wilaya ya shule ilipe gharama za elimu, ikiwa ni pamoja na elimu maalum na huduma zinazohusiana za mtoto wako mwenye ulemavu katika shule binafsi au kituo, kama wilaya ya shule imefanya elimu ya umma inayofaa (FAPE) ipatikane kwa mtoto wako na umechagua kumweka mtoto katika shule binafsi au kituo. Hata hivyo, wilaya ya shule ambapo shule binafsi inapatikana lazima imjumuishe mtoto wako miongoni mwa watu ambao mahitaji yao yanashughulikiwa chini ya vifungu vya Sehemu B kuhusu watoto ambao wamepelekwa na wazazi wao katika shule binafsi chini ya 34 CFR §§300.131 kupitia 300.144.

## *MASHARTI YA JIMBO KWA WATOTO WALIOSAJILIWA KATIKA SHULE ZA BINAFSI KWA HIARI

**K.S.A. 72-5393 and K.A.R. 91-40-43, 91-40-45, 91-40-46 and 91-40-47**

Watoto walio na upekee wanaohudhuria shule binafsi wana haki ya kupokea Elimu Inayofaa ya Umma Bila Malipo (FAPE), kupitia IEP, kutoka wilaya ya shule ambapo mwanafunzi na mzazi wanaishi, kwa ombi. Hata hivyo, kwa kushauriana na mzazi au mlezi wa mtoto na viongozi wa shule binafsi, wilaya ya shule itaamua mahali pa utoaji wa elimu maalum na huduma zinazohusiana.

- Ikiwa huduma zinatolewa katika shule ya umma, basi shule ya umma inapaswa kutoa usafiri kutoka shule ya binafsi ambapo mtoto anaenda au mahali ambapo mtoto anapokea huduma na kwenda mahali ambapo mtoto anapata huduma hadi shule binafsi au nyumbani.
- Ikiwa huduma zinatolewa katika shule binafsi, gharama za kutoa huduma zinaweza kupunguzwa kuwa gharama wastani katika wilaya ya shule kwa utoaji wa huduma sawa katika shule za umma.

Wilaya ya shule haitakiwi kutoa huduma, ikiwa ni pamoja na usafiri, nje ya mipaka ya wilaya ya shule.

Wazazi wa watoto wanaoenda shule binafsi ambao wanapokea elimu maalum na huduma zinazohusiana kulingana na IEP wanaweza kuomba usuluhishi wa elimu maalum au kuanzisha kusikia mchakato maalum wa elimu.

## TATIZO LINAPOHUSU ELIMU INAYOFAA YA UMMA BILA MALIPO

**34 CFR §300.148**

**Kurejeshewa pesa kwa masomo katika shule binafsi**

Ikiwa mtoto wako hapo awali alikuwa akipata elimu maalum na huduma zinazohusiana chini ya mamlaka ya wilaya ya shule, na ukachagua kumsajili mtoto wako katika shule binafsi, shule ya msingi, au shule ya sekondari bila idhini au rufaa ya wilaya ya shule, mahakama au ofisa wa kusikiliza anaweza kuitaka shirika husika kukufidia gharama ya usajili huo ikiwa mahakama au ofisa wa kusikiliza ataona kwamba shirika husika halikufanikisha kupatikana kwa elimu inayofaa ya umma bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako kwa wakati unaofaa kabla ya kumsajili na kwamba mtoto yupo katika shule stahiki ya binafsi. Ofisa wa kusikiliza au mahakama inaweza kuamua kuwa uamuzi wa kumsajili mtoto wako ni sahihi, hata kama usajili huo hautimizi viwango vya Serikali ambavyo vinatumika kwa elimu inayotolewa na Idara ya Elimu Jimbo na wilaya za shule.

**Ukomo wa kurejeshewa fedha**

Gharama ya kurejeshewa fedha iliyoelezwa katika aya hapo juu inaweza kupunguzwa au kukataliwa:

1. Ikiwa: (a) Katika mkutano wa hivi karibuni wa mpango mahususi kwa elimu ya mtoto (IEP) ambao ulihudhuria kabla ya kumwondoa mtoto wako katika shule ya umma, hukujulisha Timu ya IEP kwamba unakataa mazingira uliyopendekezewa na wilaya ya shule kutoa FAPE kwa mtoto wako, ikiwa ni pamoja na kueleza dukuduku lako na nia yako ya kumwandikisha mtoto wako katika shule binafsi kwa gharama za umma; au (b) Kwa angalau siku 10 za kazi (ikiwa ni

pamoja na likizo yoyote ambayo hutokea siku ya kazi) kabla hujamwondoa mtoto wako katika shule ya umma, hukutoa taarifa kwa maandishi kwa wilaya ya shule kuhusu taarifa hiyo;

2. Ikiwa, kabla ya kuondolewa kwa mtoto wako kutoka shule ya umma, wilaya ya shule ilitoa taarifa ya awali kwa maandishi ya kukusudia kumtathmini mtoto wako (ikiwa ni pamoja na taarifa ya kusudi la tathmini iliyofaa na inayoeleweka), lakini hukumpeleka mtoto wako afanyiwe tathmini; **au**

3. Mahakama ikiamua kwamba matendo yako hayakustahiki.

Hata hivyo, kurejeshewa gharama:

1. Haipaswi kupunguzwa au kukataliwa ikiwa hukutoa taarifa kama: (a) Shule ilikuzuia kutoa taarifa; (b) Hukupokea taarifa ya jukumu lako kutoa taarifa ilivyoelezwa hapo juu; au (c) Kuzingatia mahitaji yaliyo hapo juu kunaweza kusababisha madhara ya kimwili kwa mtoto wako; **na**

2. Kunaweza, kwa hiari ya mahakama au afisa wa kusikiliza, usipunguzwe au kukataliwa kwa sababu ulishindwa kutoa taarifa inayohitajika ikiwa: (a) Hujui kusoma wala kuandika au huwezi kuandika kwa Kiingereza; au (b) Kuzingatia mahitaji ya hapo juu kunaweza kusababisha madhara makubwa ya kihisia kwa mtoto wako.

Augosti 2010